Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo




## Vijana na fursa za uongozi

"Niwasihi sana nendeni mkaishi katika misingi ya uongozi kwa kuzingatia katiba, kanuni na miongozo ya chama chetu,"

Uk. 12

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00085 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Oktoba 16 - 22, 2024 |



# Dk. Samia aungwa mkono na IMF, WB




## Makamu Rais wa WB asafiri kwa Reli ya SGR

Na Mwandishi Maalum

MAKAMU wa Rais wa Benki ya Dunia (WB) anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Victoria Kwakwa, ameipongeza Tanzania kwa uwekezaji mkubwa wa mradi wa Reli ya kisasa. Uk. 4





Uk.3

## Balozi Mulamula afichua ya moyoni kuhusu Nyerere

## DC Magoti awapa saa 24 watuhumiwa kujisalimisha



Uk.2

## Madaktari Bingwa wa Samia kutua Morogoro

Na WAF, Morogoro

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, amesema Madaktari Bingwa 49 wa Rais Samia ambao wameweka kambi ya siku sita kutoa huduma za kibingwa mkoani hapa, wanatarajiwa kutatua changamoto... Uk. 5



## Hatari ya unywaji pombe kiafya

Uk.7&8


rifaly

Habarika kidijitali! Soma gazeti la Uelekeo ndani ya Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com

# DC Magoti awapa saa 24 watuhumiwa kujisalimisha

**Na Mwandishi Wetu, Kisarawe**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti, ametoa saa 24 kwa watu waliokimbia na kuacha pikipiki wakiwa wanatorosha korosho kilo 600 kutoka Kisarawe wakielekea Kibiti kujisalimisha kwa polisi kabla ya jeshi hilo halijaanza kuwasaka.

Aidha, ameonya yeyote atakayebainika akitorosha korosho kutoka wilaya hiyo kwa kutumia chombo chochote cha moto, atachukuliwa hatua za kisheria.

Alikuwa akitoa taarifa ya tukio hilo lililotokea Kata ya Marui, ambapo korosho hizo zilikuwa zikisafirishwa kwa njia za panya kwa usafiri wa pikipiki na kukamatwa juzi.

"Kisarawe hatutaki mchezo wa ujanja ujanja. Ile shoo tunayosema, ndiyo tutaanza kuwapiga hawa.

"Nimetangaza motisha ya kiasi cha Sh. 200,000 kwa yeyote atakayekamata au kubaini mtu au watu wakitorosha korosho katika Wilaya ya Kisarawe," alisema.

Alilipongeza Jeshi la Polisi, Idara ya Kilimo, na wananchi kwa kushirikiana kufanikisha kuwabaini watu hao.

"Yeyote atakayetorosha korosho, iwe kwa pikipiki, basi au daladala, korosho hizo zitataifishwa na hatua za kisheria zitachukuliwa. Huu ni uhujumu uchumi. Tumeshuhudia Rais Samia Suluhu Hassan akiwainua wakulima wadogo wa korosho.

"Tumeona huko Mtwara korosho ikiuzwa hadi Sh. 4,150 kwa kilo, lakini hapa Kisarawe wanatokea matapeli wanaowadanganya wakulima kuwa hakuna soko na wanazichukua kwa Sh. 500 hadi Sh. 800, hii haiwezekani," alisisitiza.

Mkuu huyo wa Wilaya ya Kisarawe aliongeza kuwa wakulima wanajitahidi kujiinua kimaisha kupitia kilimo cha korosho, hivyo wanahitaji kusaidiwa kuimarisha kipato chao, badala ya kudidimizwa kimaisha.



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti.

## CDF awavisha nishani maafisa wakuu, maafisa na askari JWTZ



**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi ya Wananchi wa Tanzania, Jenerali Jacob John Mkunda, kwa niaba ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia Suluhu Hassan, amewavisha nishani mbalimbali maafisa wakuu, maafisa na askari wa JWTZ jijini Mwanza.

Nishani hizo walizovishwa jana, ni ya Utumishi Uliotukuka, Nishani ya Utumishi Mrefu na Tabia Njema, Nishani ya Miaka 60 ya Muungano pamoja na Nishani ya Miaka 60 ya JWTZ.

Aidha, Jenerali Mkunda aliwavisha nishani ya Jumuiya ya SADC maafisa na askari walioshiriki Ulinzi wa Amani nchini Msumbiji chini ya mwavuli wa Jumuiya hiyo.

## Mkuu IAA kufikishwa Baraza la Maadili leo

**Na Mwandishi Wetu**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inatarajia kumfikisha mbele ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma, Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA), Profesa Eliamini Sedoyeka kwa madai ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamishna wa Maadili, Jaji Mstaafu Sivangilwa Mwangesi jana, Baraza hilo linatarajiwa kufanya kikao cha uchunguzi wa kina wa malalamiko hayo kwa mujibu wa kanuni ya 11 ya kanuni za maadili ya viongozi wa umma, mwaka 2017.

Taarifa hiyo ilisema kikao hicho kitafanyika saa 3:00 asubuhi kuanzia leo na kesho jijini Dodoma katika ukumbi wa mikutano wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.




Kamishna wa Maadili, Jaji Mstaafu Sivangilwa Mwangesi.

# Balozi Mulamula afichua yake ya moyoni kuhusu Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Kuteuliwa na Rais Balozi Liberata Mulamula, amesema anamkumbuka Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alivyothamini uchapakazi na kuwajengea uwezo watumishi wa serikali katika kutetea sera za nchi kwenye harakati za kudai uhuru.

Alisema hayo katika siku ya kumbukizi ya kifo cha Mwalimu Nyerere ambayo hufanyika kila mwaka Oktoba 14.

"Yako mambo mengi ya kumkumbuka Mwalimu, hususan, sisi tuliopata bahati ya kuhudumu serikalini kipindi chake. Binafsi namkumbuka zaidi alivyokuwa kiongozi anayetambua na kuthamini utendaji kazi na uwezo wa watendaji na wateule wake bila kujali jinsia, dini au kabila.

Alisema dhana yake hiyo ya uongozi bora, ilichochea maadili mema, utu na uzalendo mkubwa kwa wananchi.

"Mimi nikiwa Afisa wa Mambo ya Nje, kipindi hicho, Mwalimu alitufanya tujiamini katika kutetea sera yetu ya Mambo ya Nje ambayo ilijikita katika Umoja wa Afrika, harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika, kupinga ubaguzi wa rangi, kutofungamana na upande wowote katika kulinda na kutetea maslahi ya nchi yetu na watu wake na kulinda haki za binadamu.

Alisema desturi hiyo iliifanya Tanzania kuheshimika katika nyanja za kimataifa na kuwafanya wahamasike na kufanya kazi kwa bidii katika kuiwakilisha nchi nje ya nchi.


**Balozi Liberata Mulamula**


**Hayati Mwalimu Julius Nyerere**

# ASA kuongeza uzalishaji wa mbegu hadi tani 8,568

**Na Mwandishi Wetu, Tabora**

WAKALA wa Mbegu za Kilimo (ASA), unatarajia kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za kilimo kutoka tani 5,000 hadi kufikia tani 8,568 kwa msimu wa kilimo 2024/25.

Kaimu Mkurungezi Mtendaji wa ASA, Leo Mavika alisema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku tatu ya Teknolojia za Uzalishaji wa Mbegu bora za Kilimo kwa watumishi wa ASA mkoani Dodoma kupitia programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP.

Alisema kutolewa kwa mafunzo hayo ni maandalizi ya kuongeza uzalishaji wa mbegu kutoka tani 5,000 hadi kufikia tani 8,568 kwa mwaka wa kilimo 2024/25.

Alisema ongezeko la uzalishaji kwa mazao kama vile mahindi, yatazalishwa tani 2,412, alizeti tani 120, maharage tani 500, choroko tani 30, mbogamboga tani sita, ngano tani 1,500, soya tani 200, mpunga tani 1,200, mtama tani 400 na ufuta tani 150.

Mavika alisema ASA imeweka mikakati mizuri kuhakikisha inaongeza uzalishaji mkubwa ili kufikia malengo ya serikali yaliyopangwa.

Aidha, aliongeza ASA ina rasilimali ardhi ya kutosha, hivyo ina kila sababu ya kuongeza uzalishaji usiokuwa na shaka kwa maslahi ya Taifa.

Kwa upande wake, Meneja Masoko wa ASA, Angolile Mbugi, alisema mafunzo hayo yataleta mabadiliko makubwa kwa taasisi hasa katika sekta ya uzalishaji.

Aliwataka watumishi wote wa Wakala kuwa waadilifu katika uwajibikaji wao pamoja na kuepuka vishawishi vyote vinavyoweza kuharibu taswira ya Wakala.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uzalishaji, Dk. Justin Ringo, alisema maelekezo yote yaliyotolewa na Kaimu Mtendaji Mkuu, yatafanyiwa kazi kulingana na uzito wake.


**Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Dk. Zakia Mohamed Abubakar (wa pili kushoto), akiwa na maafisa wengine wa Tume katika boti akielekea Kisiwa Kidogo cha Tumbatu kilichopo Wilaya ya Kaskazini A, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar mwishoni mwa wiki, kukagua zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mjumbe huyo alitembelea vituo vinne katika Shehia za Tumbatu Jongowe, Uvuvini, Tumbatu Gomani na Mtakuja. (Picha na INEC).**

# Dk. Samia aungwa mkono na IMF, WB




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

**Na Mwandishi Maalum**

SHIRIKA la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (World Bank Group), yameunga mkono juhudi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa mapambano ya athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi kwa kuitangaza Tanzania kuwa ya pili baada ya Madagascar.

Waziri wa Fedha Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo wakati akiongoza kikao cha wataalam kutoka IMF na WB kilichofanyika ofisi ndogo ya Wizara ya Fedha mwishoni mwa wiki.

Alisema Tanzania itanufaika na Mfumo wa Ushirikiano wa Kuimarisha Hali ya Hewa kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari mbaya za uharibifu wa mazingira.

Alizishukuru taasisi hizo kubwa za fedha duniani kwa kuiteua Tanzania kuwa nchi za mwanzo duniani, zitakazonufaika na mpango huo.

Kwa upande wake, kiongozi wa timu ya wataalam kutoka IMF, Charalambos Tsangarides, alisema kupitia mpango huo, shirika hilo litaunga mkono kuanzishwa kwa kanuni za uwekezaji wa umma zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na utoaji taarifa.

Aidha, alisema WB itajikita kusaidia kutekeleza miradi katika sekta zitakazoimarisha uwezo wa Tanzania kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama vile nishati, maji, hifadhi ya jamii na kilimo.

Kupitia Mfumo huo, IMF na WBG watafanya kazi kwa karibu na washirika wengine wa maendeleo, kuratibu juhudi zao za kuunga mkono ajenda ya mageuzi ya sera ya Tanzania ili kukabiliana na vihatarishi na changamoto zinazohusiana na mabadiliko hayo ya tabianchi na kuimarisha ustahimilivu wa uchumi wa Tanzania.

Alisema taasisi hizo mbili pia zitasaidia uboreshaji na utekelezaji wa sera ya Tanzania ya usimamizi wa hatari za maafa, ikiwa ni pamoja na kufadhili mfumo wa kukabiliana na hatari hizo na uimarishaji wa mtandao wa usalama wa kijamii ili kukabiliana na majanga ya hali ya hewa.

IMF na WBG pia zitasaidia sera za kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji, kupanua upangaji na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji, kusimamia vihatarishi vya hali ya hewa katika uchumi na fedha na kutoa msaada wa kiufundi na kifedha kwa kuishirikisha pia sekta binafsi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkazi wa WB, Nathan Belete, akizungumza kwa njia ya mtandao kutoka Washington D.C, nchini Marekani, alisema Tanzania itanufaika na msaada wa kiufundi na kifedha kutoka taasisi hizo mbili katika kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa miundombinu itakayokuza uzalishaji, kuhifadhi mazingira na kuwa na mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi.

# Makamu Rais wa WB asafiri kwa Reli ya SGR

## ● Ateta na Dk. Mwigulu Nchemba ufadhili vipande SGR vilivyosalia

**Na Mwandishi Maalum**

MAKAMU wa Rais wa Benki ya Dunia (WB) anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Victoria Kwakwa, ameipongeza Tanzania kwa uwekezaji mkubwa wa mradi wa Reli ya kisasa inayotumia umeme (SGR).

Alisema mradi huo utakuwa kichocheo kikubwa cha usafirishaji wa abiria na mizigo na kuchangia ukuaji wa uchumi si tu kwa Tanzania bali kwa nchi zote za Ukanda wa Maziwa Makuu.

Alisema hayo wakati akisafiri kwa reli hiyo kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma akiwa pamoja na Afisa Mwandamizi wa benki hiyo, Makiko Watanabe katika ziara ya siku tatu nchini.



Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia (WB) anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Victoria Kwakwa (kushoto) na Afisa Mwandamizi wa benki hiyo, Makiko Watanabe.

Victoria alikuwa nchini kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na WB.

Katika ziara hiyo, alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba kuhusu ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwa ni pamoja na uwezekano wa benki hiyo kushiriki katika ufadhili wa vipande vya SGR vilivyosalia.

"Mradi huo utakuwa kichocheo kikubwa cha usafirishaji wa abiria na mizigo na kuchangia ukuaji wa uchumi si tu kwa Tanzania bali kwa nchi zote za Ukanda wa Maziwa Makuu.

# Madaktari Bingwa wa Samia kutua Morogoro



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima

**Na WAF, Morogoro**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, amesema Madaktari Bingwa 49 wa Rais Samia ambao wameweka kambi ya siku sita kutoa huduma za kibingwa mkoani hapa, wanatarajiwa kutatua changamoto za kiafya zinazowakabili wananchi.

Aidha, amesema uwepo wa Madaktari Bingwa hao katika hospitali za halmashauri siyo jambo la kisiasa, bali ni jambo kubwa la kuokoa maisha na kuboresha afya za wananchi.

Alisema hayo alipowapokea madaktari hao ofisini kwake mwishoni mwa wiki.

Alisema wananchi wa mkoa huo wana uhitaji wa huduma za matibabu ya kibingwa, hivyo uwepo wa kambi hiyo ni mkombozi kwao katika kutatua changamoto zao za kiafya.

“Nimshukuru Rais Dk. Samia kwa kuwasambaza madaktari bingwa hawa katika hospitali zetu za halmashauri lakini pia nimshukuru Waziri wa Afya Jenista Mhagama kwa kutekeleza maelekezo ya Rais, kazi mnayokwenda kuifanya madaktari bingwa kuwahudumia wananchi ni kazi kubwa mno, mjue sisi wana Morogoro tunawahitaji, tunawathamini na tunawapenda,” alisema.


Awali, akimkaribisha Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Mussa Ali Mussa, aliahidi ushirikiano kwa kipindi chote Madaktari Bingwa hao watakapokuwa mkoani hapa.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi ili kupata huduma hizo za kibingwa zilizosogezwa karibu na maeneo yao.

Akitoa salamu za Wizara ya Afya Mratibu wa Kambi Mkoa wa Morogoro Dk. Ismail Mohammed Mtitu alisema lengo kubwa la kupeleka Madaktari Bingwa wa Rais Samia ni kusogeza huduma za kibingwa karibu na wananchi ili kupunguza gharama za matibabu na kuondoa rufaa, kuanzisha wodi za kuhudumia watoto wachanga pamoja na kutoa mafunzo elekezi kwa wataalam waliopo katika hospitali za halmashauri.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi





## Ongezeni wingi safari za SGR

Bado imekuwa ni nadra mtu anayetaka kusafiri kwa kutumia treni ya kisasa (SGR) kupata tiketi siku hiyohiyo. Unaweza kujaribu hata sasa kupata usafiri wa leo jioni, bila shaka utakuta kwamba tiketi zimejaa.

Wakati wa uzinduzi wa treni hiyo ya kisasa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli, Masanja Kadogosa alikaririwa akisema kwamba kadri watu watakavyokuwa wanaongozeka kutumia usafiri huo, wingi wa treni za kufanya safari na mabehewa yataongezeka pia. Lakini ni kama imeshindikana.

Ni vyema ifikie wakati mtu asilazimike kubuku safari ya SGR siku mbili tatu bali hata sasa mtu akiamua kusafiri leo apate usafiri huo wa haraka na rahisi kama ilivyo kwenye mabasi. Hali hii ya treni mpaka ubuku siku mbili tatu inaweza kukaribisha ulanguzi wa tiketi.




MAONI YA MHARIRI

## Tushiriki uchaguzi serikali za mitaa kwa manufaa yetu

JUMATATU ya wiki hii, katika hafla ya kilele cha kuhitimisha Mbio za Mwenge wa Uhuru jijini Mwanza, Rais Samia Suluhu Hassan alisisitiza umuhimu wa kila Mtanzania mwenye sifa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Rais ametoa wito kwa Watanzania kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kuchagua viongozi bora kwenye ngazi za vijiji, kata na mitaa na kwamba wasichukulie uchaguzi huo kwa uzito mdogo.

Rais Samia anabainisha kuwa uchaguzi huu ni sehemu muhimu ya kuimarisha demokrasia nchini na kuchangia maendeleo ya maeneo yetu kwa kuchagua viongozi wenye uwezo wa kutatua changamoto zinazotukabili katika ngazi hizi za chini.

Uchaguzi huu, ambao umepangwa kufanyika Novemba 27, 2024, utaweka viongozi wapya kwenye nafasi za wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa serikali za mitaa na wenyeviti wa mitaa.

Rais Samia anasema kwamba uchaguzi wa serikali za mitaa unatoa nafasi kwetu wananchi kushiriki katika kuamua mwelekeo wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo yao.

Tunaungana na Rais Samia kuhimiza wananchi kujiandikisha ili kuweza kushiriki kwenye uchaguzi huu muhimu kwa kuzingatia, kama alivyosema kwamba uchaguzi wa serikali za mitaa unatoa nafasi kwa wananchi kushiriki moja kwa moja katika maamuzi yanayohusu maendeleo ya maeneo yetu.

Hii ni fursa adhimu ya sisi wananchi kupata watu wa kuwakilisha maslahi yetu kwa ufanisi zaidi.

Kupitia uchaguzi huu pia inatupa wasaa wa kuwawajibisha viongozi wa mitaa yetu ambao tuliwachagua katika kipindi kilichopita lakini wameshindwa kutekelezi majukumu yao kama tulivyotarajia. Hivyo ni wasaa wetu wa kuwapiga chini na kuchagua viongozi wapya.

Uchaguzi huu pia utawezesha maendeleo ya mitaa yetu kwa maana kwamba viongozi wa serikali za mitaa huchaguliwa kwa madhumuni ya kusimamia shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika maeneo yetu.

Kupitia uchaguzi huu, ni fursa kwetu wananchi kuchagua viongozi wenye uwezo wa kuleta mabadiliko chanya, kuanzisha miradi ya maendeleo pamoja na kuboresha huduma za kijamii kama afya, elimu na maji safi.

Faida nyingine ya kushiriki uchaguzi huu ni ukweli kwamba serikali za mitaa zinahusika na usimamizi wa huduma za msingi zinazotugusa wananchi moja kwa moja. Na kupitia uchaguzi huu tutakuwa tumehusika kuweka viongozi wenye dhamira ya kuboresha utoaji wa huduma hizo kwa kuzingatia mahitaji ya jamii yetu.

Kwa kuwa serikali za mitaa ni kiungo kati ya serikali kuu na wananchi, uchaguzi huu unasaidia pia kuimarisha uhusiano huo kwa viongozi wa mitaa huwasilisha kero na mahitaji yetu kwa serikali kuu.

Kwa ujumla, uchaguzi wa serikali za mitaa ni chombo muhimu cha kuimarisha utawala bora, kuleta uwajibikaji na kuchangia maendeleo endelevu, hivyo ni muhimu sana kila mwenye sifa kushiriki.

Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255784122020
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com

Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

## Hongera Chadema kutambua umuhimu wa SGR

WAZARAMO wana usemi wao unaonena kuwa; "Usiongee ukamaliza". Hapa walimaanisha ruksa kuongea, lakini kumbuka kuweka akiba ya maneno!

Wiki iliyopita, Oktoba 11 viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) walitumia kwa mara ya kwanza usafiri wa treni ya kisasa (SGR), ukipenda iite ya Mwendokasi wakati wa safari yao kutoka Dar es Salaam kuelekea Dodoma.

Katika safari hiyo, viongozi hao wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika pamoja na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, walionesha kuridhishwa na huduma za usafiri wa SGR.

Viongozi hao pia wamepongeza utekelezaji wa mradi huo, wakieleza kuwa, sio kila mradi wa serikali unapaswa kupingwa, kwani baadhi ya miradi, kama huu wa SGR, unaleta manufaa kwa wananchi. Wameeleza kuwa mradi huo ni wa kihistoria na unatekelezwa kwa ufanisi mkubwa, hivyo unastahili kuungwa mkono.

> **Sio kila mradi wa serikali unapaswa kupingwa, kwani baadhi ya miradi, kama huu wa SGR, unaleta manufaa kwa wananchi. Wameeleza kuwa mradi huo ni wa kihistoria na unatekelezwa kwa ufanisi mkubwa, hivyo unastahili kuungwa mkono.**

Pia viongozi hao wa Chadema walitoa maoni kuhusu filamu ya 'Royal Tour' inayooneshwa ndani ya treni za Mwendokasi kuwa, hatua hiyo ni ya kipekee katika kuhamasisha utalii, kwani filamu hiyo inawavutia abiria wengi, wakiwemo wageni na hivyo kuhamasisha idadi ya watalii nchini.

SGR ni reli ya kisasa na ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, inayotumia nishati ya umeme na yenye uwezo wa kupitisha treni zenye mwendo kasi wa kilomita 160 kwa saa.

Mradi huu unalenga kuboresha sekta ya usafirishaji nchini Tanzania na kuongeza ufanisi katika huduma za usafiri wa reli.

Kauli hizi zinazotolewa hivi sasa na viongozi wa Chadema ni tafauti walizokuwa wanatoa awali wakati Serikali ilipotangaza mkakati wa ujenzi wa mradi huu mkubwa hapa nchini na Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

Ikumbukwe mradi huu wa SGR ulikwenda sambamba na ununuzi wa ndege mpya wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya hayati, John Pombe Magufuli na aliyekuwa Makamu wake wa rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, lakini wahafadhina hawa wa Chadema waliipinga miradi yote hiyo miwili kwa maneno makali na ya kebehi!

Walisema ni matumizi mabaya ya fedha za serikali zinazotokana na kodi za wananchi sambamba na kudai iligubikwa na harufu ya rushwa katika utekelezaji wake!

Hivi sasa Watanzania wameanza kula matunda ya uwekezaji wa mradi huu wakiwemo Wanachadema wote na viongozi wao waliokuwa wanaupinga awali, sasa wamegeuka kama vinyonga na kumwaga pongezi!

Sasa ndiyo wanakurupuka na kukumbuka shuka wakati kumeshakucha kwa kukiri kwamba, si kila mradi wa serikali unapaswa kupingwa! Kweli maneno ya Wazaramo yalikuwa na maana sana; "Usinene ukamala!"

# Hatari ya unywaji pombe kiafya



MAENEO mengi duniani, karamu itakuwa haijakamilika bila kuwepo pombe.

Aidha, baadhi ya watu unywaji wa pombe huwa ndiyo ni njia nzuri ya kuanzisha mazungumzo na watu wengine asiowafahamu.

Mara nyingi, watu hunywa pombe kwa ajili ya kusherehekea, kujumuika, kujiliwaza au kuondoa mawazo.

Baadhi ya tafiti miaka ya nyuma zilisema kuwa matumizi ya wastani ya baadhi ya pombe kama ile nyekundu, inaweza kuwa nzuri kiafya.



Hata hivyo, sasa Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema hakuna kiwango salama cha unywaji pombe kwa afya ya binadamu.

Wanaume hutumia karibu mara nne zaidi ya pombe kuliko wanawake.

Kwa mujibu wa WHO, Unywaji wa pombe huchangia vifo vya watu milioni 2.6 duniani kote kila mwaka.

Pombe husababisha aina saba za saratani ikiwemo saratani ya utumbo na matiti.

Utafiti wa kina wa WHO uligundua, hata unywaji mdogo na wa wastani wa pombe, yaani chini ya lita 1.5 ya mvinyo au chini ya lita 3.5 ya bia au chini ya mililita 450 za pombe kali, ni hatari kwa afya.

Mwongozo mpya wa WHO unasema hakuna kiasi salama na hatari kwa afya ya mnywaji huanza na tone la kwanza la kinywaji chochote cha kileo.

Takwimu za WHO pia zinaonesha kuwa jumla ya unywaji wa pombe kwa kila

Inaendelea uk. 8

> **Utafiti wa kina wa WHO uligundua, hata unywaji mdogo na wa wastani wa pombe, yaani chini ya lita 1.5 ya mvinyo au chini ya lita 3.5 ya bia au chini ya mililita 450 za pombe kali, ni hatari kwa afya.**

# Hatari ya unywaji pombe kiafya

Inatoka uk. 7

mtu duniani kote, umepungua kidogo kutoka lita 5.7 mwaka 2010 hadi lita 5.5 mwaka 2019.

Wanaume ni wanywaji wakubwa na hutumia wastani wa lita 8.2 ikilinganishwa na lita 2.2 za wanawake kwa mwaka.

Dk. Tim Stockwell, ni mwanasayansi katika Taasisi ya Utafiti wa Matumizi ya Dawa za Kulevya kutoka Canada na anasadikisha kuhusu usahihi wa onyo la WHO.

"Pombe kimsingi ni kemikali hatari na ni hatari mara tu unapoanza kuinywa."

Alifanya uchambuzi wa kisayansi wa tafiti mia moja na saba, ili kupata uhusiano kati ya unywaji pombe na kifo.

Ikiwa kuna hatari ya kifo kimoja kati ya watu 100 inapewa lebo ya wastani na kifo kimoja kati ya watu 1,000 inapewa lebo ya chini ya hatari, linasema jarida la British Medical Journal.

Serikali ya Uingereza inapendekeza kunywa si zaidi ya uniti 14 kwa wiki, ambayo ni karibu glasi sita za wastani za mvinyo au bia.

Stockwell anasema wazo kwamba unywaji pombe wa kiasi ni nzuri lilikuja kwa sababu ya mbinu duni za utafiti.

Maswali hayakuwa ya kitaalamu. Na baadhi ya mambo muhimu yalipuuzwa.

**WANYWAJI WANASEMAJE?**

Walevi wengi huona ni vigumu mno kuacha kunywa.

Lakini siyo kila mtu hufikiria hatari zinazohusiana na pombe ni jambo kubwa.

"Kwa kweli sielewi msisitizo huu wa kujaribu kuelewa hatari za kunywa kinywaji kimoja au viwili kwa siku," anasema Profesa Sir David Spiegelhalter.

Yeye ni Profesa Mstaafu wa Takwimu katika Chuo Kikuu cha Cambridge nchini Uingereza, anaelezea jinsi ambavyo tunaweza kuzielewa hatari.

"Hakuna kiwango salama cha kuendesha gari. Hakuna kiwango salama cha kuishi, lakini hakuna mtu anayependekeza kuacha. Tunahitaji kuangalia kubadilisha madhara kuwa faida."

Dk Spiegelhalte ana shaka kuhusu uwezo wetu wa kukadiria hatari kwa usahihi.

"Nadhani tunapaswa kukubali tu kwamba watu wanakunywa ili kufurahia."

Huku akisisitiza kuwa yeye si sehemu ya watu wanaoshawishi unywaji wa pombe wala kushawishi watu kuwa na kampeni dhidi ya pombe.

Aliambia BBC kwa nini anafurahia unywaji wa kiasi.

"Hatari inamaanisha inapunguza wastani wa umri





> **Zaidi ya miaka hamsini ya kunywa, kinywaji hicho kwa wastani kwa siku, kitachukua muda wa miezi sita tu ya maisha yako au kupunguza dakika kumi na tano kila siku.**

wa kuishi kwa asilimia moja."

"Zaidi ya miaka hamsini ya kunywa, kinywaji hicho kwa wastani kwa siku, kitachukua muda wa miezi sita tu ya maisha yako au kupunguza dakika kumi na tano kila siku."

Dk. Spiegelhalte anataja hata kutazama TV kwa saa moja kwa siku au kula mkate wa nyama ya nguruwe, mara mbili kwa wiki pia kuna hatari za kiafya.

Na anataka watu wazima wafanye uamuzi wao wenyewe kuhusu yale yanayowafaa.

Dk. Tim Stockwell, pia anafurahia kinywaji chake na hapendekezi kuacha kunywa.

"Ukinywa pombe, kitu cha kufurahisha sana, ingawa ina hatari kidogo kwa afya yako."

BBC.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

| Jumatano Oktoba 16 - 22, 2024 |

UTALII

AFYA

JAMII

Jarida hili haliuzwi



# Vijana na fursa za uongozi Tanzania

UK. 12 & 13



# Maigizo ya sasa dhidi ya uongozi wa Dk. Samia Suluhu si mageni

**Na Mwandishi Wetu**

"TUWE makini. Kuna watu wasioitakia mema serikali. Wanaratibu na kufadhili mambo ya hatari sana. Kwani hamshangazwi na hili wimbi la wanamuziki kutunga nyimbo za ajabu ajabu? Hamshangazwi pia na maigizo ya utekaji nyara? Mnadhani haya yanatokea tu? Kuna watu wana hasira sana na serikali hii na wamejipanga ndani na nje ya nchi… Lakini hatimaye watashindwa."

Maneno haya yaliwahi kusemwa na mwandishi mmoja mkongwe kipindi cha uongozi wa Rais John Magufuli kwenye kundi moja sogozi la mtandao wa whatsapp. Kwa ujumbe huo, kuna waliomwelewa anachomaanisha, kuna ambao hawakumwelewa kabisa na kuna waliomwelewa lakini wakamkejeli.

Tangu aingie madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan amefanya makubwa, akiendeleza yale aliyoyafanya Mtangulizi wake na kuibua mapya ambayo katu hayawezi kumwacha bila kuwa na maadui wengi, na hasa ikizingatiwa kwamba baadhi ya maadui hawa wamejaaliwa "kuchonga maneno" na wengine wana uwezo mkubwa wa kifedha na mbinu mbalimbali chafu. Na hii yote ni ubinafsi tu ambayo ni moja ya tabia za binadamu.

Tukumbuke kwamba tangu aingie madarakani, kuanzia wakati akiwa na Hayati Magufuli na sasa akiwa na Makamu wake, Mchumi Dk. Phillip Mpango, Rais Samia amefilisi kabisa ajenda za wale waliokuwa wakipigia kelele za ufisadi, matumizi mabaya ya madaraka, ukwepaji wa kodi na uwajibikaji duni katika sekta ya umma.

Badala yake wanashuhudia kasi ya ajabu ya maendeleo huku akija na mambo kadhaa muhimu sana kwa wananchi kama kumtua mama ndoo, kueneza umeme kila kijiji, kuja ni mpango wa kumwondoa mwanamke kwenye matumizi ya nishati chafu, kuwaingiza vijana kwenye kilimo cha kisasa (BBT), kuibuka na mpango wa kupeleka madaktari bingwa sehemu mbalimbali za nchi, kuja na mpango wa Bima ya Afya kwa wote, kumalizia miradi yote ya kimkakati kama SGR, Bwawa la Mwalimu Nyerere na mengineyo lukuki.

Na hapa sijazungumzia na kudadavua kwa kina falsafa ya R4 aliokuja nayo Rais Samia ambayo pamoja na kuwapa ahuweni kubwa wapinzani na kuwa mwelekeo mzuri sana kwa mustakabali wa nchi yetu, wapinzania wametaka kuitumia vibaya falsafa hiyo wakidhani sasa wanaweza kufanya wanayotaka hata kama ni mambo yanayohatarisha amani ya nchi!

Huko nyuma ajenda za wapinzani wa serikali ya CCM zilikuwa na mashiko kwa sababu kulikuwa na ukweli fulani wa hali hiyo. Matendo hayo waliokuwa wakiyapigia makelele yalikuwa yamegeuka kuwa kama utamaduni kwa walio wengi na hali ilikuwa imefikia kama isiyoweza kuhimilika.

Baada ya Samia kuingia madarakani kuanzia zama akiwa na mwenda zake JPM, yale ambayo wengi waliyapigia makelele hayapo na hivyo kuwafilisi ajenda hiyo wapinzani. Haraka sana tuliona sura zao halisi kwamba kumbe kelele zao hazikuwa halisi bali kutudanganya tu Watanzania kwani hawajapatapo kuunga mkono juhudi ambazo zimekuwa zikifanyika. Nashangaa kuona majuzi wakisifia SGR baada ya kusafiri nayo!

Nakumbuka Mosese Machali aliyekuwa mmoja wa walioshindwa unafiki wa kutounga mkono juhudi zinazofanywa na serikali, aliwahi kusema yafuatayo:

"Ni jambo la ajabu na aibu kwa watu makini na wenye kuhitaji mabadiliko ya kweli kuacha kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali… Mimi Moses Joseph Machali, niliyefanya sana siasa za upinzani hapa nchini na niliyepiga kelele na kupinga siasa za kifisadi zilizoitawala nchi hii; niliyepinga pia ufisadi uliokuwa umeitawala serikali huko nyuma kwa nguvu na uwezo wangu wote nikishirikiana na wapinzani wenzangu, ninaamua kujiunga na watu wanaonesha dhamira safi ya kuiendeleza nchi yetu. Watu wenye mwelekeo na dhamira ya kujenga nchi yetu kwa maendeleo endelevu ni jamii ya akina Magufuli, Kassim Majaliwa na kadhalika.

"Kwa kushirikiana na wapinzania wenzangu enzi hizo tulishauri na kupinga ufisadi wa kila aina, tuliitaka serikali kufanya mambo yenye tija kwa taifa na sasa kila mwenye macho anaona hatua zinazochukuliwa na serikali.

Machali alisema taifa hili haliwezi kuendelea kwa kuwa na siasa za kutokukubaliana na ukweli unaoishi. Akasema kama dhamira ya kila Mtanzania ikiwemo wapinzani ni kuona nchi inasonga mbele basi hatuhitaji kuwa watu wa kupingapinga hata yaliyo mema bali kuyaunga mkono yale yaliyo mema bila kujali yanafanywa na nani…"

La msingi ni kwamba Watanzania si wajinga, wanajua na wanaona namna Rais Samia anavyowapa maendeleo makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kama ilivyokuwa wakati wa JPM baada ya kufilisi ajenda za wapinzani kubwa ikiwa ya kusubiri serikali ikosee wapate cha kusema na tatizo la ufisadi na wajibikaji duni watendaji, kwa wanaokumbuka, kulikuwa na maigizo mengi ya utekaji nyara na nyimbo za wanamuziki wa kizazi kipya katika kuiaminisha jamii kwamba mambo hayako sawa. Haya ndio yanayotokea sasa hasa tunapokuwa tunaelekea kwenye chaguzi zetu. Hamjashtuka tu?

Ninachoamini ni kwamba watashindwa kwa sababu nyingi. Kwanza ni wachache, watandanganya 'weee' lakini ukweli utakuwa unadhihiri punde. Watawayumbisha sana Watanzania ikiwa ni pamoja na kuwaambia maisha ni magumu lakini Watanzania hawatakawia kuona manufaa kama wanayoendelea kuyaona sasa ya kusomesha watoto wao bure, kununuliwa ndege mpya na kufufua ATCL, kuanza kutumia reli ya uhakika, Kanda ya Ziwa, mbali na kupata meli mpya kuona daraja la Magufuli linaanza kupitika na kadhaika.

Lakini kikubwa zaidi ni kwamba watashindwa kwa sababu Mungu hatokuwa upande wao, abadani. Hii ni kwa sababu Rais Samia ana nia njema na wao wana nia ovu.

# Bwawa la Mindu 'linavyokauka' na kuleta adha ya maji Morogoro

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni kulikuwa na habari, hasa kwenye mitandao ya kijamii, ya baadhi ya wananchi wa Manispaa ya Morogoro kulalamika kwamba wanapata maji kwa nadra katika maeneo yao.

Taarifa ilikuwa kana kwamba kuna uzembe mahala fulani unafanyika lakini uchunguzi unaonesha kwamba hali ya upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro ni kizungumkuti, na hivyo ni kuombea mvua zinyeshe ili hali ibadilike!

Lakini kubwa ambalo jamii inapaswa kujifunza kutokana hili kwa sababu ndio chanzo cha hali inayoukumba Mji Kasoro Bahari ni uharibifu wa mazingira hasa kwa kuzingatia kwamba Morogoro ni eneo ambalo liko karibu na Dar es Salaam na ambalo ukataji wa miti kwa ajili ya kupata nishati chafu ya mkaa umekuwa ukifanyika sana mbali na shughuli za kilimo na ufugaji.

Kabla ya hatua ya sasa ya kujaribu kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, asilimia zaidi ya 70 ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam walikuwa wanatumia mkaa na jiji hilo lilikuwa linatumia zaidi mkaa kulinganisha na mikoa mingine nchini.

Uchunguzi unaonesha makali ya mgawo wa maji Morogoro yanaongezeka siku hadi siku, hatua inayopelekea maeneo mengi mjini humo kupata maji mara moja kwa wiki.

Kutokana na malalamiko, Mwandishi wa Makala haya amezunguka kwenye viunga vya mji wa Morogroro na kujionea misururu mirefu ya akina mama wakiwa na ndoo zao za maji wakisubiri kuchota maji kwenye vituo vya kuchotea maji.

"Adha ya maji ni kubwa. Mitaani kumeenea vituo vya kuchote maji, lakini maji hayatoki siku zote. Yanatoka siku moja kwa wiki na yanapotoka tunalazimika kuja kwenye vituo vya kuchotea maji saa 10 usiku kuwahi foleni ndefu inayotupelekea kushinda vituoni kutwa nzima," anasema Afsa Chasamba, mkazi wa mtaa wa Kilongo B, Kata ya Mkundi.

Naye Leah Juma Mkazi wa Lukobe, anasema kuwa hali ya upatinaji wa maji mtaani kwao ni mbaya. Maji yanatoka mara moja kwa wiki hivyo kwa mtu ambaye hana vyomb vingi ya kuhifadhia maji hujikuta ndani ya siku mbili hana maji!

"Tunanunua maji ndoo safi ya kunywa shilingi 500. Maji haya ambayo yanasambazwa na MORUWASA (Mamlaka ya Maji na Usafi na Mazingira Morogoro) yakiisha tunalazimika kununua maji kwa wauzaji binafsi, ndoo shilingi 500. Hii inatuongezea ugumu wa maisha," anasema

Anasema kuwa kutokana na ugumu huo wa upatikanaji wa maji, wanalazimika kutumia maji ya visima ambayo yana chumvi nyingi na kwamba wanayatumia kwa ajili ya kufulia, kuoga na kuoshea vyombo.

"Haya maji ya MORUWASA tunayatumia kwa kunywa tu. Shughuli nyingine zote tunatumia maji ya kwenye visima ambayo pia hatuna uhakika kama hayana madhara kwa afya zetu," anasema.

### CHANZO CHA TATIZO

Uchunguzi umebaini kuwa uhaba huo wa maji katika Manispaa ya Morogoro unatokana na vyanzo vya maji ambavyo ni mito inayoingiza maji kwenye Bwawa la Mindu kukauka katika msimu huu wa kiangazi.

Bwawa la Mindu ambalo linatumika kama chanzo kikuu cha kusambaza maji mjini Morogoro linategemea kujazwa na mito midogo ya Mgeta, Mto Mzinga, mto Mlali, Mto Ngerengere na mto Lukurunge.

Mito hiyo kwa sasa baadhi inatiririsha maji kwa kiasi kidogo sana huku mto ambao ni tegemezi wa kuingiza maji bwawa la Mindu, yaani Mto Mlali ukiwa umekauka kabisa.

Uchunguzi zaidi umebaini kuwa katika miaka ya karibuni, mito hiyo hujaa wakati wa masika lakini wakati huu wa kiangazi hukauka kutokana na maji hayo, licha ya uchache wake, hutumika kwa shughuli za kibiniadamu kama vile kumwagia mashamba sambamba na uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vyake kutokana na shughuli za binadamu.

"Miaka ya nyuma mito hii ilikuwa inatiririsha maji kwa msimu wa mwaka mzima. Kwa sasa mito hii imekuwa mito ya msimu, ndiyo sababu wakati wa masika hakuna shida ya maji lakini wakati wa kiangazi, hali inakuwa mbaya," anasema Mzee Joseph Mkude, mkazi wa Forest mjini Morogoro.

Mzee Joseph anasema kuwa sababu za mito hiyo kutotirirsha maji kwa msimu yote ya mwaka ni uharibifu wa mazingira katika Milima ya Urugulu.

"Mito hii yote inatoka kwenye kilele cha milima ya Uruguru, sasa hebu tazama hali ilivyo kule mlimani, ni kipara. Hakuna tena msitu mnene, maeneo mengi watu wamejenga na wanalima," Alisema.

Kinachoonekana ni kwamba endapo kiangazi kitaendelea na mvua za vuli zikachelewa kunyesha, Mji wa Morogoro utakuwa hatarini kukumbwa na uhaba mkubwa wa maji safi na salama ya kunywa kuliko hata ilivyo sasa.

### KAULI YA MORUWASA

Mwandishi wa makala haya amepiga hodi ofisi za Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (MORUWASA) na kufanikiwa kuzungumza na Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Tamimu Katakweba.

Katakweba anakiri kuwa maji mjini Morogoro kwa sasa yanatolewa kwa mgao katika baadhi ya maeneo huku kukiwa na jitihada kubwa za serikali kupitia mamlaka hiyo kuendelea kuboresha huduma hiyo muhimu kwa ustawi wa biniadamu.

Anasema kuwa mamlaka hiyo ina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 41 kwa siku lakini kwa sasa wanazalisha lita milioni 37 huku mahitaji ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro kwa siku yakiwa lita milioni 81.

Katakaweba anasema hali ya sasa inachangiwa na Bwawa la Mindu kutokuwa na maji ya kutosha msimu huu wa kiangazi kwa kuwa bado ndio chanzo pekee cha maji mjini Morogoro.

Anasema mikakati ipo ya kuboresha huduma za maji katika mji wa Morogoro ambayo ni pamoja na kuongeza kina cha bwawa la Mindu ambalo kwa sasa lina uwezo wa kuhifdhi maji lita bilioni 11.3 tu. Anasema kwa kuliongezea kina linawe uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 22.8 sambamba na kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya maji.

Anataja mpango mwingine ambao tayari umeanza kutekelezwa kuwa ni kutafuta maji chini ya ardhi ambapo tayari wameanza kuchimba visima virefu eneo la Dakawa Wilayani Mvomero.

Katakweba anasema kuwa hayo yote yatafanikiwa ikiwa wananchi wataendelea kutunza mazingira ili kuhifadhi vyanzo vya maji.

"Tuyatunze mazingira yetu kwa wivu mkubwa, kwa kuwa juhudi zote ambazo serikali inazifanya ikiwa ni pamoja na kutafuta maji chini ya ardhi, kuongeza uwezo wa kuhifadhi maji Bwawa la Mindu, hazitazaa matunda endepo kama mazingira yatendelea kuharibiwa," anasema.

### MAMBO YA KUFAHAMU

Katika kufikia nini kifanyike kuokoa mito na mabwawa mengine nchini likiemo Bwawa la Mindu, mambo yafuatayo yuanapaswa kuzingatiwa.

Ukataji miti na ukataji wa misitu: Sehemu za vyanzo vya mito zimekuwa zikiharibiwa kutokana na shughuli za kilimo, ukataji wa miti hovyo, na matumizi ya ardhi yasiyo endelevu. Hii husababisha mmomonyoko wa ardhi ambao huleta mchanga mwingi kwenye mito, na hivyo kupunguza uwezo wa bwawa kuhifadhi maji safi.

Kilimo kandokando ya mito na migodi: Shughuli za kilimo karibu na mito na uchimbaji wa madini hasa dhahabu karibu na mito ni shughuli zenye madhara pia kwa mustakabali wa mito ikiwa ni pamoja na kuharibu kingo za mito na uoto wa asili.

Ufugaji holela: Ufugaji wa mifugo kando ya mito husababisha uharibifu wa kingo za mito na kupelekea mmomonyoko wa udongo pamoja na uchafuzi wa maji kutokana na taka za mifugo.

Kuongezeka kwa makazi ya watu: Ukuaji wa miji na makazi kando ya mito unachangia uharibifu wa mazingira, kwani watu hujenga karibu na vyanzo vya maji bila kufuata sheria za uhifadhi wa mazingira, na hivyo kuathiri mito inayopeleka maji kwenye Bwawa la Mindu.

### MAMBO YA KUFANYA

Mbali na juhudi za kutafuta vyanzo vingine vya maji kama inavyofanya Moruwasa, kubwa ni viongozi kusimamia ipasavyo Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ambayo pamoja na kanuni zake inataka shughuli za kilimo zifanyike umbali wa mita 60 kutoka kwenye kingo za mito au vyanzo vya maji. Hii inajumuisha kilimo, ujenzi na shughuli nyinginezo ambazo zinaweza kuharibu kingo za mito au kuchafua maji.

Sheria pia inataka muhimu wa kuhifadhi kingo za mito iwe ni ya msimu au ya kudumu, ili kuzuia mmomonyoko wa udongo na uchafuzi wa maji. Lingine ni uhifadhi wa misitu kandokando ya mito ambapo sheria inahimiza uhifadhi wa uoto wa asili karibu na mito.

Lakini pia ni muhimu kuunga mkono juhudi za Rais Samia ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.






# Vijana na fursa za uongozi Tanzania

Na Hamid Yassin

JOTO la uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwezi ujao, Novemba 27 linazidi kupanda huku vijana wengi wakihusishwa kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uongozi badala ya kutumika kama wapiga debe wa wanasiasa wakongwe.

Vyama vya siasa na watia nia hawako nyuma kwenye harakati na taratibu za kuelekea kwenye tukio hilo muhimu kabisa kwa mustakabali wa taifa letu.

Leo imenipendeza kuzungumzia zaidi nafasi ya vijana kwenye jambo hili. Vijana ni kundi muhimu, adhimu na la kimkakati sana kwenye uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa, kwani ukiachana na wingi wao mkubwa ndani ya nchi lakini zaidi vijana ni kundi linalotazamwa kwa umakini sana na vyama vya siasa na watia nia ya kugombea.

Kipindi hiki kuelekea uchaguzi wanasiasa wengi karata na akili zao ziko sana kwa vijana ili wapate wa kuwapa nguvu na kuwaunga mkono.

Vijana wanalengwa sana na wanasiasa kwa sababu ni kundi linaloweza kuamua mshindi wa nafasi yoyote ya uongozi kwenye uchaguzi kutokana na wingi wao.

Wanasiasa nyakati hizi za kuelekea uchaguzi wanahaha sana kuwatafuta vijana wanaoweza kuwaunga mkono ili waweze kushinda.

Kipindi hiki wanasiasa wanajitahidi mno kuwa karibu na vijana kwenye mambo yao mbalimbali ili wapate nguvu yao kuelekea kwenye uchaguzi.

Ni jambo la kawaida sana kwa wanasiasa kuelekea kipindi hiki cha uchaguzi kusikia wakianzisha mashindano mbalimbali ya michezo ya vijana, kusaidia vikundi mbalimbali vya vijana, vikoba na kuwafikia vijana kwenye maeneo yao ili kusikiliza kero zao kama njia ya kuwashawishi vijana wawaunge mkono. Vijana nyakati hizi ni kama dhahabu ing'aayo mbele ya wanasiasa.

Nyakati hizi kwa vijana ni zaidi ya kitendawili kinachosubiri kutenguliwa.

### SASA NI WAKATI WAO VIJANA

Baada ya kutumika kama ngazi kwa wanasiasa waliobobea na wakongwe, naamini sasa ni wakati wa vijana nao kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu na kuwakabili wanasiasa waliotangulia miaka mingi nyuma.

Vijana kwa uwingi na ushawishi wao mkubwa kwenye uchaguzi wakifanya makosa na kukubali kuendelea kutumika kwa wanasiasa wengine, hususani wale wanaotumia nguvu ya fedha zao kupata uongozi basi, hawatakuwa na wa kumlaumu zaidi ya kuzisuta nafsi zao wenyewe.

Vijana wakatae kutumika na badala yake wawe na ajenda moja kuelekea uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa ya kujitokeza kugombea kote nchini.

Si dhambi wala ubaya kwa vijana kuwaunga mkono wanasiasa wengine kwenye uchaguzi, lakini ni muhimu zaidi kwa vijana kutafakari kwa undani wanasiasa wanaowaunga mkono wa kuwaachia kugombea.

Vijana waangalie watu wenye maono kweli ya kutaka kuiona Tanzania inasonga mbele. Wanasiasa wenye historia nzuri kwenye jamii na maisha yao ya kila siku. Wanasiasa wenye hamu na hoja shawishi zinazotekelezeka kwenye maeneo yao.

Vijana wakiwaunga mkono wanasiasa wabobevu kwa

sababu ya hongo ya aina yoyote ile ama ahadi za kuwabeba hapo baadaye, basi watakuwa wameliangusha na kutolitendea haki taifa lao hili.

**MANENO 'KUNTU' YA KAWAIDA**

Julai11 hadi 17, 2024, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), Mohammed Ali Kawaida, aliwasihi viongozi wa umoja huo kuanzia ngazi ya mikoa na wilaya zote nchini, kujifunza namna ya kuishi kwenye misingi ya uongozi kwa vitendo huku wakizingatia katiba, kanuni na miongozo ya Chama Cha Mapinduzi.

Pia aliwataka viongozi hao ambao walishiriki mafunzo ya Chuo cha Umoja huo, Ihemi mkoani Iringa, kuhamasisha ushiriki wa vijana kikamilifu katika uandikishaji katika Daftari la Kudumu la Wapigakura lililofungiliwa rasmi Julai 20, 2024 mkoani Kigoma sambamba na hili zoezi lililoanza juzi la kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa wa mwezi ujao.

Kawaida aliyasema hayo alipokuwa anahutubia viongozi na watendaji wa UVCCM katika ufungaji wa mafunzo ya viongozi na watendaji wa umoja huo mikoa na wilaya zote nchi nzima yaliyofanyika Ihemi mkoani Iringa.

"Niwasihi sana nendeni mkaishi katika misingi ya uongozi kwa kuzingatia katiba, kanuni na miongozo ya chama chetu," alisema na kuongeza.

"Nimefurahishwa sana namna ambavyo mmekuwa wasikivu, mmeishi kwa ushirikiano, mmeishi kwa umoja na kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika kipindi chote cha mafunzo yenu. Mmedhihirisha kuwa ninyi ni viongozi wa kweli na mmekuwa katika misingi ya uongozi ndani ya CCM."


Aidha, aliwasisitiza kudumisha ushirikiano wa viongozi wa umoja huo wa Vijana wa CCM na viongozi wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu katika maeneo yao. Kawaida alisema ni vema viongozi hao wakafuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama na kutangaza kazi nzuri zinazofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika maeneo yao.

Akizungumzia Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Kawaida alisema viongozi lazima wawe mstari wa mbele katika kuhamasisha vijana wenzao aweze kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwani 2025.

**VIJANA NI TAIFA LA LEO**

Naam; baada ya tabaruku hiyo ya Mwenyekiti wa UV-CCM, Komredi Kawaida, hebu nirudi kuwazungumzia hawa vijana ambao siku hizi wamegoma kabisa kuitwa 'Taifa la kesho! Na mimi ninakubaliana nao kwamba vijana ni taifa la leo na kesho

Mimi binafsi sielewi hii kauli ya vijana kuitwa 'Taifa la kesho' ilitoka wapi! Nani alianzisha na kwa masilahi ya nani na yepi? Kwani hata waasisi wa taifa hili



akina hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wenzake wakati wanapigania uhuru wa taifa hili kutoka kwa wakoloni, hawakuwa wazee, bali vijana wabichi kabisa!

Lakini sisi wazee tuliozaliwa baada ya uhuru tumeikuta hii kauli mbiu ya 'Vijana taifa la kesho' na tumeishi nayo hivyo hivyo hadi kizazi hiki cha sasa ambacho kimekuja kuikataa kabisa tena kwa vitendo!

Siyo kwamba tu siku hizi vijana wanahimizana kushiriki katika chaguzi mbalimbali za nchi, lakini ukweli ndiyo wamesheheni kwenye nafasi za uongozi wa taifa hili hivi sasa!

Na wengi wao wameonesha kumudu mikiki ya kupigania maendeleo ya taifa hili. Ama kwa maneno mengine ni kwamba hawajawaangusha waliowaamini!

Nawapongeza vijana wanapohimizana kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi yetu. Nasema kuwapongeza kwa sababu kiukweli mwaka huu umefua dafu kulinganisha na miaka mingine kwa vijana kuhimizana kuwania nafasi za uongozi tangu uhuru wa taifa hili.

**ANGALIZO KWENU VIJANA**

Hata hivyo, niweke angalizo kwamba si kila kijana ana uwezo au anafaa kuongoza kwani wapo ambao uwezo huo hawana na wapo wanaodhani uongozi ni kuukata au kwenda kutumia uongozi kwa maslahi binafsi.

Vijana wanaopaswa kupendekezwa kugombea na vijana wenzao ni wale ambao wanaonesha uadilifu na utayari wa kuitumikia nchi yao. Yaani vijana wazalendo na wanaotambua kwamba uongozi uongozi ni utumishi, uongozi ni mzigo. Kwamba unapokuwa kiongozi basi matatizo yote ya wale unaowaongoza ni mzigo wako!

Kwa msingi huo, vijana msimfumbie macho kijana mwenzenu ambaye anataka kugombea uongozi, hata kama ni rafiki yenu kiasi gani, kama mnajua uzalendo wake, uadilifu wake na maono yake ni ya kutilia mashaka.

**HONGERA DK. SAMIA**

Hata hivyo, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na safu yake yote kwa kuwa chachu kubwa katika hatima hiyo ya kuona vijana wakifurika kuwania uongozi wa taifa hili adhimu hapa duniani.

Nasema "kwa kuwa chachu kubwa" kwa sababu hakuna ubishi hata chembe kwamba Rais Samia amewafumbua watu na hasa vijana macho kuwania uongozi; Na hii ni zawadi ya Manani kwetu kwa mtu ambaye ni mzalendo kwa watu wake.

Ki vipi? Ndiyo; kwa sababu siku zote kiongozi anabeba msalaba mkubwa kuhakikisha watu wake wananeemeka katika kipindi chake cha uongozi.

Kana kwamba hiyo haitoshi ni kiongozi huyo huyo ndiye anayeweka msingi mkubwa wa maendeleo ya wananchi wake tangu ya kijamii hadi ya kitaifa.

Msingi huo lazima uende sambamba pasipo kuchuja kwa wananchi hao ambao siku zote ndiyo walinzi wa taifa lao.

Pamoja wimbo ule wa kwamba Vijana ni 'Taifa la kesho', haimaanishi huko nyuma hakukuwa na viongozi vijana, walikuwepo wengi miaka ya mwanzo ya uhuru lakini kadiri miaka ilivyosonga ndivyo nao walipungua kwa kasi na kubaki wazee wengi wakishika hatamu ya kuongoza taifa hili.

**NYERERE NI MFANO MZURI KWENU**

Nasema si jipya kwa sababu, Baba wa Taifa hayati Mwalimu Nyerere aliweka msingi huu tangu akipigania uhuru wa nchi hii kuanzia mwaka 1954 yeye na wenzake walipoanzisha chama cha kupigania uhuru wa Tanganyika cha The Tanganyika African National Union (TANU).

Mwalimu, akiwa kijana wakati huo, akawa muwazi kabisa kuhakikisha mapambano yale yalifanywa na wote bila kujali kabila zetu, asili zetu, dini zetu wala ukanda wetu.

Wazee wote walimshangaa lakini kadri siku zilivyokuwa zikisonga mbele walianza kumkubali na hatima yake wakakubali yeye apewe uongozi wa Taifa hili mwaka 1961 akiwa kijana wa miaka 39 tu.

Mwalimu alionesha thamani ya usomi wake, ujana wake, taaluma yake na thamani ya wazazi wake achilia mbali jamii na taifa la Tanganyika wakati huo hadi ilipoungana na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania.

Huu ndio ulikuwa ujana wa thamani na wa kheri kubwa kwa taifa hili na baadaye Afrika nzima kutokana na msimamo wake wa kuhakikisha watu wanakuwa huru ndani ya nchi yao na viongozi si wa nchi hizo tu bali pia Afrika nzima.

Mwalimu Nyerere alishirikiana na vijana wenzake wa Afrika wa wakati huo kama kina-Nkwame Nkurumah, Muamar Sadat, Ahmed Sekou Toure, Patrice Lumumba, Abubakar Tafawa Balewa na wengine wengi kulikomboa Bara hili kutoka kwenye makucha ya wakoloni.

Mwalimu huyo huyo akaifanya nchi yake ya Tanzania kuwa kitovu cha uhuru wa Bara la Afrika pale alipowakaribisha hapa nchini wapambanaji kama vile kina Samora Machel, Robert Mugabe na wengine wengi kwa ajili ya kujipanga na mapambano ya kuzikomboa nchi zao.

Kilichomfanya Mwalimu kujitosa katika hili ni kile alichokisema ambacho kinaishi hadi leo hii. Naomba nimnukuu; "Tanzania haitakuwa huru kama jirani zake watakuwa bado wakitawaliwa".

Tunaliona hili leo likifanywa na rais wetu, Dk. Samia pale anapoufufua na kuuimarisha ushirikiano wa kimataifa wa Tanzania na mataifa mengine ndani na nje ya Bara hili la Afrika.

Ni wazi bila ubishi kuwa Dk. Samia anafuata nyayo za Baba wa Taifa katika kuliwezesha hili na leo hii Tanzania imerejea katika upendo mkubwa uliopotea wa nchi hizo na nyingine nje ya Afrika.

Lakini kwa nini Dk. Samia anakuwa msitari wa mbele katika masuala haya ya maendeleo ya kijamii, uchumi na uhusiano na nchi hizo? Ndiyo; yote hiyo ni kwa sababu Rais wetu huyu anaijua historia ya Afrika na dunia nzima.

Ni kwa msingi huu basi ndipo ninapokuja kwa dhati kabisa kusema kuwa vijana wetu watakaojitokeza kuwania uongozi lazima tuwapime kama wanaijua historia ya nchi hii na Afrika bila kusahau ya dunia.

Ni muhimu sana vijana wawe kama Mwalimu Nyerere ambaye aliutumia ujana wake vyema kiasi cha wazee wenyewe wakiwemo viongozi wa dini, kumkubali na kuwa naye bega kwa bega kuelekea uhuru wa Taifa hili na Afrika nzima.

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.*

Hamid Yassin

# Mwl. Julius Nyerere kioo cha dunia!

BABA wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alidhihirisha kuwa yeye ni kioo cha dunia kutokana na wanazuoni, wanafalsafa, wanataaluma, viongozi na watu mbalimbali duniani kutamani kufuata nyayo zake kwa udi na uvumba katika fikra zake, maoni yake, mtazamo wake na utekelezaji wa maisha yake hapa duniani.

Juzi Jumatatu Mwalimu Nyerere alitimiza miaka 25 tangu aage dunia mnamo tarehe 14, Oktoba, 1999 na kuacha mtazamo ambao kila kiongozi, wana majimui, wana historia, wapenda amani na utulivu duniani wakibaki wanashangaa na maono yake ambayo wengine wakati ule hawakumwelewa ila sasa ukweli umedhihirika kuwa ni kioo cha dunia kila mmoja inabidi ajitazame kupitia yeye.

Mwalimu Nyerere aliteka tafakuri za wengi kwa kujitoa kwake kwa hali na mali na kupenyeza fikra zake kwa Watanzania wote kuwa na wajibu wa kusaidia, kuwaunga mkono na kupambana ana kwa ana na wadhalimu na wanaokandamiza uhuru wa mtu yeyote hapa duniani, mfano hai wa kupigania uhuru wa Bara la Afrika.

Juhudi za Baba wa Taifa kutetea wanyonge, kupigania umoja, amani, haki na usawa, hazikuishia tu hapa nchini, zilivuka hadi nje ya mipaka ya nchi yetu. Tanzania, chini ya uongozi wa Mwalimu, ilikuwa mstari wa mbele kwenye harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Ilikuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya Nchi Huru za Afrika (OAU) na pia ilitoa hifadhi na mafunzo kwa vyama vya ukombozi vya Afrika Kusini, Angola, Msumbiji, Namibia na Zimbabwe, hadi nchi hizo zilipopata uhuru.

Kama hiyo haitoshi, hata Rais Yoweri Museveni wa Uganda aliwahi kukiri hadharani kuwa, bila Mwalimu Nyerere huenda yeye asingekuwa Rais wa Uganda hivi sasa.

Mbali na kutoa mchango kwenye harakati za ukombozi, Baba wa Taifa alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa OAU, sasa Umoja wa Afrika, na pia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Tanzania pia chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere, ilikuwa mtetezi wa haki za wanyonge duniani kote.

Mathalan, tulikuwa mstari wa mbele kutetea haki ya Jamhuri ya Watu wa China kupata uanachama kwenye Umoja wa Mataifa. Zaidi ya hapo, Mwalimu Nyerere alishiriki kwenye usuluhishi wa migogoro Barani Afrika. Na katika kudhihirisha hilo, wakati anafariki dunia alikuwa Msuluhishi wa mgogoro wa Burundi.

Huyo ndiye Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; Mpigania Uhuru, Mwanamajumui halisi (Pan-Africanist), mpenda amani, haki, umoja na usawa; Rais wa TAA na TANU.

Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyekiti wa kwanza wa CCM; Baba wa Taifa letu, ambaye leo tunakumbuka kifo chake na kusheherekea maisha yake.

Kwa ujumla, naweza kusema kuwa, Mwalimu Nyerere alikuwa miongoni mwa viongozi bora kuwahi kutokea sio tu hapa nchini, bali pia Barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Vijana na watoto wetu hawana budi kumfahamu mtu huyu wa aina yake katika historia ya nchi. Tuwafundishe watoto wetu fikra za Mwalimu Nyerere. Tuwasimulie kazi na mambo aliyoyasimamia kwa Watanzania wote kwa ujumla, hatuna budi kuenzi mambo mazuri aliyotuachia Baba wa Taifa letu.

Aidha, Mwalimu Nyerere alijitolea kwa ajili ya wanyonge, ambapo alisukumwa na upendo kwa Taifa lake kwa faida ya wananchi wote mfano alikubali kuacha mshahara wake wa ualimu ili atumike katika shughuli za chama chake kwa faida ya Watanzana wote na kuhakikisha anaikomboa Tanganyika 09 Disemba 1961.

Mwalimu Nyerere hakutoa upendeleo wala kuendekeza ubinafsi kwake wala kwa familia yake bali alihimiza kufyekelea mbali matabaka ya kiuchumi, kabila au kikanda alitilia mkazo watu wote kuheshimiana licha ya tofauti zao za kidini kinasaba au kikabila. Aidha, Mwalimu Nyerere alikuwa mpole kupokea marekebisho pale alipokosolewa na zaidi sana alitoa msamaha kwa wale waliomkosea kwani kwake kukosa na kukosoana ni sehemu ya maisha ya binadamu.

Akizungumzia Mwalimu Nyerere katika mchakato wa ujenzi wa Taifa la Tanzania Profesa Antonio Pooda, Mhadhiri kutoka katika Kitivo cha Misiolojia Urbaniana, alimwita Mwalimu Nyerere kuwa ni 'Mbuyu' akitafsiri dhana kwamba ni mtu muhimu aliyetoa mchango wake mkubwa katika harakati za kuelimisha Watanzania na Afrika kiujumla kutumia akili zao wenyewe kubuni mifumo ya kujitegemea na kujikwamua katika wimbi la umasikini, ujinga na maradhi maadui nambari moja.

Prof. Pooda aliongeza Mwalimu Nyerere hakutaka Tanzania kuwa nakala ya taifa lingine lolote bali taifa halisi (original) lililo huru na linalojitawala katika maamuzi ya utendaji wake kuwahudumia watu wake, katika hili elimu ni ufunguo muhimu ili kufahamu mahitaji halisi ya taifa na kutengeneza mifumo stahiki kwa wakati na nafasi iliyopo.

Mnamo tarehe 14, Oktoba, 2013 Mwangalizi wa kudumu wa Muungano wa Nchi za Afrika Kwenye Umoja wa Mataifa, Antonio Tete, alimtaja Hayati Mwalimu Nyerere kama mtu anayekumbukwa kama kiongozi wa Ukombozi wa Afrika.

Akiongea wakati wa kuadhimisha Siku ya Mwalimu Julius Nyerere, ambayo imeadhimishwa kwa mara ya kwanza kwenye Umoja wa Mataifa, mwaka huo Tete alimsifu Mwalimu Nyerere kama kiongozi aliyekuwa mwadilifu, jasiri na shujaa wa uhuru wa Afrika.

"Kama kiongozi mwenye busara, Mwalimu alichangia sana katika mjadala kuhusu pengo la maendeleo ya kiuchumi baina ya mataifa ya Kaskazini na yale ya Kusini mwa dunia. Hafla hiyo ilikuwa muhimu kwa sababu ilikwenda sambamba na maadhimisho ya uzinduzi wa Umoja wa Afrika, ambao Mwalimu alichangia sana kama mmoja wa waanzilishi wake," alisema Tete.

Aliongeza kuwa Mwalimu Nyerere alipigania uhuru wa nchi za Afrika na haki ya kijamii. Alikuwa kielelezo cha uongozi kwa nchi zote za Afrika katika mapambano yao ya uhuru na hamu ya amani, uhuru na maendeleo ya kiuchumi."

Akizungumza katika kongamano la Kigoda cha Mwalimu Nyerere wakati wa kumbukizi ya miaka 18 bila Mwalimu Nyerere, Mwanasheria Nguli wa Kenya, Prof. Patrick Lumumba, ambaye alionesha kwa kuchambua udhaifu na mema ya viongozi kadhaa wa Afrika, alisema Waafrika wengi wanahitaji maendeleo yanayogusa maisha yao na si vingine.

"Mwafrika anataka chakula kizuri, shule, hospitali nzuri na ajira kwa vijana, tunataka viongozi watakaoboresha miundombinu, kilimo, maisha ya wanawake na watoto," alisema Prof. Lumumba.

Aliongeza kuwa viongozi wengi wa Afrika wamekuwa wakiendesha siasa chafu, kujilimbikizia mali, wala rushwa, kutokuwa tayari kujisahihisha na kuendekeza ukabila.

Mwalimu Nyerere amesema "Ili tuendelee tunahitaji viti vinne; Watu, Ardhi, Siasa safi na Uongozi bora, hii ni kweli kabisa nasema:

"Hakuna siasa safi Afrika, kwa miaka 30 viongozi wanaotawala wamekuwa mafisadi na wabinafsi lakini mfumo unawapa fursa za kuendelea kuwa wachafu.

Nchi inaweza kujiita ya demokrasia kama Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) lakini haina demokrasia na leo hii ni kati ya nchi ambazo ni maskini," alisema.

Alibainisha kuwa Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa na maono makubwa kwani aliipenda nchi yake na hata alipofanya makosa alitambua na kujisahihisha.


"Nyerere aliwahi kusema Ikulu ni mahali patakatifu lakini wako baadhi ya viongozi wakiondoka madarakani wanakuwa wamejilimbikizia mali na wengine hukutwa na mabilioni katika akaunti zao. Huyu ni mtu aliyewaunganisha watu wa makabila tofauti na kuwa taifa moja na kuzungumza lugha moja," alisema Prof. Lumumba.

Aidha, ameongeza kuwa kama ukabila hautapigwa vita utaendelea kuangamiza mataifa mengi na kutolea mifano ya nchi za DRC, Msumbiji, Zambia, Somalia, Nigeria, Kenya na Ethiopia.

"Suala la ukabila bado ni tatizo, Tanzania ina bahati kubwa kwa sababu Mwalimu Nyerere alijenga misingi imara ambayo inastahili kuigwa. Kenya ukijaribu kumuuliza mgombea atafanya nini pindi atakapochaguliwa anakwambia mimi ni Mluo na sasa ni zamu yetu, wengine unamuuliza rais wa awamu ya tatu ni nani anakujibu kuwa ni Uhuru na ni Mkikuyu tunataka aendelee kutawala... Mungu aisaidie nchi yangu (Kenya)," aliongeza.

Hakika Mwalimu Nyerere ni Kioo Cha Dunia kwani ushawishi wake, upendo wake wa kujitolea na kuwatumikia watu duniani ulisababisha nchi nyingi kukubali kushiriki kwa njia moja au nyingine kusaidia harakati za uhuru na ukombozi wa nchi nyingi Barani Afrika kama vile, Urusi, China, Cuba na nchi za Scandinavia (Norway, Dernmark, Finland, Iceland na Sweeden).

Mfano nchi ya Norway ilishiriki kujenga makambi ya wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika eneo la Mazimbu Morogoro na Dakawa.



*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Seneti itamwacha salama Naibu Rais wa Kenya?

BAADA ya Naibu Rais, Rigathi Gachagua kushindwa kuzima mpango wa kuwasilishwa kwa hoja ya kumwondoa madarakani katika Seneti, sasa hatima yake iko mikononi mwa maseneta 67 wa bunge hilo.

Akikataa ombi la jopo la mawakili wa Gachagua, wakiongozwa na Paul Muite, Jaji wa Mahakama Kuu Lawrence Mugambi aliagiza kuwasilishwa kwa kesi zote 22 zinazopinga kung'atuliwa kwa kiongozi huyo kwa Jaji Mkuu, Martha Koome ili ateue jopo la majaji watatu kuzisikiliza na kuziamua.

Alisema kesi hizo zinaibua masuala mazito ya kikatiba na yanayosheheni masilahi ya umma na hivyo yanapasa kuamuliwa na zaidi ya jaji mmoja.

Jaji Mugambi alitoa uamuzi huo Ijumaa iliyopita, siku tatu baada ya Bunge la Kenye kupitisha hoja ya kumtimua Gachagua madarakani na siku moja baada ya Spika wa Seneti, Amason Kingi kuagiza kuwa hoja hiyo itashughulikiwa na maseneta mnamo Oktoba 16 na Oktoba 17 (yaani leo Jumatano na kesho Alhamisi).

Kwenye taarifa yake, Kingi pia alipiga marufuku safari zozote za maseneta na wafanyakazi wa asasi hiyo nje ya nchi kuhakikisha kuwa maseneta wote wanashiriki katika mijadala na upigaji kura kuamua hatima ya hoja hiyo.

Aidha, alikataza kufanyika kwa vikao vyovyote vya Seneti nje ya Nairobi kati ya Oktoba 8 hadi 19 mwaka huu.

"Mjuavyo, Seneti itahitaji kufanya maamuzi kuhusu shughuli muhimu siku zijazo. Kulingana na uzito wa suala hili, ni muhimu kwa maseneta wote kuwepo na kushiriki," alisema Spika huyo wa Seneti katika taarifa hiyo.

"Kwa hivyo safari za maseneta na maofisa wa seneti nje ya nchi zimesitishwa," Kingi akaongeza.

Kulingana na kipengele cha 150 (2) cha Katiba ya Kenye kuhusu hitaji la kuondolewa afisini kwa Naibu Rais, hoja ya kufanikisha hatua hiyo inapasa kuungwa mkono na angalau theluthi mbili ya maseneta wote 67 wakiwemo maseneta maalumu.

Isitoshe, tofauti na hoja za kuwaondoa afisini magavana ambazo hupigiwa kura na maseneti 47 wanaowakilisha kaunti pekee, hoja kama hii itapigiwa kura na maseneta wote 67, wakiwemo maseneta maalumu.

Kwa hivyo, kesho Alhamisi hoja hiyo inahitaji kuungwa mkono na angalau maseneta 45 ndipo ipite na hivyo kumfanya Gachagua kukoma kuendelea na wadhifa wa Naibu Rais.

Kwa upande mwingine, ili hoja hiyo isipite, Gachagua atahitaji kuungwa mkono na angalau maseneta 23 kwani hitaji la kikatiba la theluthi mbili ya maseneta halitati,ia.

Wadadisi wanasema, kwa kuzingatia jinsi wabunge walivyopigia kura hoja hiyo Oktoba 8, itakuwa kibarua kigumu kwa Naibu Rais kupata uungwaji mkono kutoka idadi hii ya maseneta.

Upigaji kura katika Bunge la Kitaifa ulionesha pia kwamba masuala la kivyama na kimaeneo yalihusika au kuzingatiwa katika kumng'oa Gachagua.

Kwa misingi hiyo, inabashiriwa kuwa huenda maseneta 51 wakaunga mkono hoja hiyo huku 12 wakiipinga. Kwa upande mwingine, msimamo wa maseneta wengine wanne haujabainika.

"Ni wazi kuwa maseneta wa chama cha UDA na ambao ni waaminifu kwa Rais William Ruto wataunga mkono hoja hiyo. Aidha, maseneta wa ODM ambao bila shaka ni waaminifu kwa Waziri Mkuu wa zamani Raila Odinga pia wataunga mkono hoja hiyo. Hili lilishuhudiwa katika Bunge la Kitaifa na bila shaka linarejelewa katika Seneti siku ya Alhamisi," anasema mchambuzi wa masuala ya kisiasa na uongozi, Barasa Nyukuri.

"Kwa hivyo, nafasi ya Gachagua kupona shoka la Seneti ni finyu mnamo. Sababu ni kwamba kwa kiwango kikubwa huu ni mchakato unaoshawishiwa pakubwa na siasa wala sio sheria au uzito wa mashtaka. Tulishuhudia hili wakati wa kuondolewa ofisini kwa gavana wa zamani wa Nairobi, Mike Sonko na Ferdinand Waititu wa Kiambu," anaongeza.

Ilivyo sasa, chama cha UDA kinachoongozwa na Rais Ruto kinawakilishwa na jumla ya maseneta 34 katika Seneti huku ODM ikiwa na maseneta 20.

Vyama vya Wiper na Jubilee vinawakilishwa na maseneta wanne kila kimoja, United Democratic Movement (UDM) ina maseneta wawili huku vyama vya Democratic Party, Ford Kenya na National Reconstruction Alliance (NRA) vikiwakilishwa na seneta mmoja kila kimoja.

Kiongozi wa Wiper ameamuru maseneta wanne wa chama hicho kutokuunga mkono hoja hiyo ili kumnusuru Gachagua. Wao ni Enoch Wambua (Kitui), Daniel Maanzo (Makueni), Agnes Kavindu (Machakos) na Seneta Maalum, Shakila Abdallah.

Maseneta wa UDA ambao ni wandani wa Gachagua na hivyo wanatarajiwa kutokuunga mkono hoja huyo ni James Murango (Kirinyaga), Karungo Wa Thang'wah (Kiambu), Joe Nyutu (Murang'a) na John Methu wa Nyandarua.

Kuna uwezekano mkubwa kwamba Seneta wa Busia, Okiya Omtatah wa chama cha NRA atapinga hoja hiyo pia ikizingatiwa kuwa amepinga mchakato huo tangu ulipoanza.

Maseneta ambao misimamo yao haujulikani ni pamoja na Tabitha Karanja (Nakuru), John Kinyua (Laikipia), Wahome Wamatinga (Nyeri) na Samson Cherargei wa Nandi.

Makosa 11 yaliyowasilishwa Bungeni dhidi ya Gachagua ni pamoja na madai ya ufisadi, kutumia vibaya madaraka na ukiukaji wa katiba.

Baadhi ya tuhuma maalumu kwa Naibu Rais ni kuchochea ukabila, ubaguzi, na kusababisha mgawanyiko wa kitaifa. Kwa mfano, Gachagua anatuhumiwa kwa kutoa matamshi ya kuchochea kwamba miradi ya maendeleo nchini Kenya inapaswa kugawiwa kwa misingi ya jinsi watu walivyopiga kura katika uchaguzi mkuu wa 2022, jambo linaloonekana kuvuruga umoja wa kitaifa.

Aidha, mashtaka mengine yanahusiana na matumizi mabaya ya mamlaka na ukiukwaji wa vipengele mbalimbali vya katiba ya Kenya. Pia anadaiwa kufanya mambo ambayo yanamdhalilisha au kumdunisha bosi wake, yaani Rais William Ruto.

Wabunge wengi waliunga mkono hoja ya kumwondoa madarakani, na hatua inayofuata itakuwa mbele ya Seneti, ambapo mashtaka haya yatapitiwa kwa kina ili kutoa uamuzi wa mwisho

Wakati wa kura za wabunge kuhusu hoja ya kumwondoa Naibu Rais madarakani, wabunge 281 waliunga mkono mashtaka dhidi yake, huku 44 wakipinga hoja hiyo. Mbunge mmoja aliamua kutochagua upande wowote.

Katika hatua nyingine Rais William Ruto Jumapili iliyopita alikkwepa kuzungumzia masaibu yanayomwandama Naibu wake huku akisema lengo lake ni kuhakikisha kuwa taifa lina umoja na usawa kwa wote.

Rais alizungumzia Bima mpya ya Afya (SHA) ambayo alisema itasaidia kufanikisha mageuzi katika sekta ya afya na mradi wa nyumba za gharama ya chini.

Hiyo ilikuwa mara ya pili kwa Rais kukwepa kuzungumzia masuala na tuhuma zinazomhusu Gachagua.

*Chanzo: Taifa Leo na mitandao ya kompyuta*





## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Ubia kama wa Temesa na sekta binafsi muhimu

SERIKALI peke yake haiweza kutatua changamoto zote za wananchi bila kushirikiana na sekta binafsi (Public and Private Partnership-PPP) kutokana na ukweli kuwa sekta binafsi imara ni kichocheo kikubwa cha maendeleo.

Jambo la kushukuru na kupongeza ni kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imeipa msukumo na mkazo wa kipekee sekta binafsi ili iweze kuwa kiungo muhimu katika juhudi za kuimarisha maendeleo ya wananchi.

Sekta binafsi ina umuhimu mkubwa katika kushirikiana na serikali kwa sababu inachangia ukuaji wa uchumi, ubunifu, na ufanisi katika utoaji wa huduma za umma. Hapa ni baadhi ya vipengele vya umuhimu wa sekta binafsi:

Mosi ni uchochea Ukuaji wa Uchumi: Sekta binafsi huchangia kwa kiasi kikubwa kwenye uzalishaji wa mali, ajira, na mapato ya kodi, hivyo kuongeza pato la taifa na kuimarisha uchumi wa nchi. Ushirikiano na serikali unaweza kusaidia sekta hii kuwa na mazingira bora ya kuwekeza na kupanua shughuli zake.

Pili, ubunifu na Ufanisi: Sekta binafsi ina uwezo wa kuleta ubunifu na teknolojia mpya, ambazo zinaweza kuongeza ufanisi katika miradi ya umma kama miundombinu, afya, na elimu. Serikali ikishirikiana na sekta binafsi inaweza kupunguza gharama na kuboresha ubora wa huduma.

Tatu, uwekezaji katika miundombinu: Kupitia ushirikiano na sekta binafsi, serikali inaweza kupata rasilimali za kifedha na utaalamu wa kitaalamu kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu kama vile barabara, madaraja, na nishati. Hii ni muhimu kwa sababu serikali mara nyingi inakabiliwa na changamoto za bajeti ndogo.

Nne, kukuza Ajira: Sekta binafsi inaongoza katika kuzalisha ajira, hivyo ushirikiano kati ya sekta hii na serikali unaweza kusaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa kuwa na mazingira yanayofaa kwa ukuaji wa biashara.

Tano, kuziba pengo la huduma za umma: Katika maeneo ambayo serikali haiwezi kutoa huduma kwa kiwango kinachotakiwa, sekta binafsi inaweza kuingilia na kusaidia kutoa huduma hizo, kama vile afya, elimu, na huduma za kijamii.

Kukabiliana na changamoto za kijamii: Kwa ushirikiano, sekta binafsi na serikali zinaweza kushughulikia changamoto kama vile umaskini, mabadiliko ya tabianchi, na maendeleo ya kiuchumi kwa njia ya miradi endelevu.

Kwa ujumla, ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali unalenga kuboresha maisha ya watu kwa kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia nguvu ya pamoja na rasilimali.

Hivyo ni muhimu kwa wizara, idara, wakala na vitengo kuipa msukumo sekta binafsi badala ya kutegemea makusanyo yao, ruzuku kutoka serikali kuu au wakati mwingine mikopo kwa ajili ya kuibua na kujenga miradi mbalimbali. Ni vyema wakaimarisha ubia na sekta binafsi ili kuharakisha maendeleo ya wananchi kwani umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Niwapongeze Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kwa kwa kutambua umuhimu wa sekta binafsi na hivyo kuishirikisha katika utoaji wa huduma za karakana, vivuko na ukodishaji mitambo ili kuboresha huduma bora kwa wananchi.

Temesa ni wakala wa serikali wenye wajibu wa kufanya matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo ya serikali. Pia, Temesa inawajibika katika uendeshaji wa vivuko vya serikali na kukodisha mitambo hasa ile ya ujenzi wa miundombinu ili kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Taarifa ya Temesa inasema; "Temesa inasimamia mitambo ya karakana 30 katika mikoa yote 26 nchini ambazo kwa wastani zinahudumia magari takribani 29,263 kwa mwaka. Pia, Temesa inakarabati na kuhudumia magari ya serikali yapatayo 9,183, pikipiki 12,778 na vifaa au mitambo 433. Aidha, Temesa inaendesha vivuko 32 katika mikoa 12 na maeneo ya kuvuka 22 kote nchini huku takribani abiria 79,863 na magari 3,696 wakipita katika vivuko hivi kila siku."

Huduma ya usafirishaji ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanafika katika maeneo yao ya kazi na hivyo kushikiki kikamilifu katika ujenzi wa taifa kupitia shughuli zao za uzalishaji mali. Pia, serikali inahitaji vyombo ya usafiri kama magari, vivuko na pikipiki katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuwahudumia na kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa hiyo, panapokuwa na mkwamo wa huduma za usafiri, wananchi na serikali hupata hasara na hivyo tija ya uzalishaji inakosekana, ndiyo maana ni muhimu huduma za usafiri ziimarishwe ili kuchochea maendeleo.

Temesa kupitia karakana zake inayo dhamana ya kutengeneza vyombo vya usafiri pale vinavyoharibika na kupata hitilafu ili kuvirejesha katika hali yake nzuri ili kutoathiri utoaji wa huduma kwa wananchi.

Taarifa ya Temesa inaendelea kusema "Katika nia za kuimarisha ufanisi na ubora, Temesa imedhamiria kuendesha karakana zake 13 kwa njia ya ubia. Karakana hizo ziko katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Shinyanga, Kagera, Singida, Iringa na Mara. Mikoa mingine ni pamoja na Manyara, Pwani, Lindi, Ruvuma, Njombe na Simiyu. Vilevile Wakala unakusudia kuendesha huduma zote za vivuko nchini kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP)."

Karakana na vivuko bora ni muhimu katika kuhakiksiha huduma bora zinatolewa kwa wananchi. Ongezeko la watu na mahitaji ya huduma unaifanya Temesa pekee kushindwa kuhimili utoaji wa huduma bora kwa serikali na wananchi wake. Hivyo basi, msingi wa ubia wa serikali na sekta binafsi ni nyenzo muhimu ya kuimarisha utoaji wa huduma bora na kuchagiza maendeleo hasa kijamii na kiuchumi.

Taarifa ya Temesa inasisitiza; "Mpango wa Temesa wa kuboresha karakana zake, vivuko na kutoa huduma ya ukodishaji mitambo kwa njia ya ubia unatoa matumaini ya kukidhi mahitaji makubwa ya huduma hizi yaliyopo kwenye soko. Ushirikishwaji wa wawekezaji utaleta manufaa mengi ikiwepo kuvutia teknolojia za kisasa, kuchochea ufanisi wa uendeshaji wa karakana na vivuko pamoja na kuboresha ubora wa huduma za wakala kwa ujumla wake."

Sekta ya ujenzi na miundombinu kwa ujumla imepewa msukumo mkubwa na serikali kutokana na umuhimu wake kimaendeleo. Sekta hizi zinahitaji uwepo wa mitambo mikubwa na vifaa vya kisasa ili kukidhi viwango vya ujenzi wa miradi na miundombinu mbalimbali kama vile barabara na madaraja.

Temesa inamiliki mitambo 41 kwa ajili ya kukodisha kwa wateja kwenye sekta za umma na binafsi, Mitambo hii haitoshi kutokana na mahitaji makubwa yaliyopo sasa. Hivyo basi, ubia baina ya Temesa na sekta binafsi kwa maana ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi utawezesha ununuzi wa mitambo mikubwa na ya kisasa inayoweza kukidhi mahitaji na ubora wa miradi inayotekelezwa nchini ili kutoa huduma bora. Aidha, mitambo hiyo itaweza kukodishwa kwa wakandarasi mbalimbali ili kutekeleza miradi na hivyo kuongeza tija kimaendeleo.

Kuhusu Temesa kushirikisha sekta binafsi, Kamishna wa PPP, David Kafulila amesema; "Mpango wa Temesa kuboresha karakana zake na kutoa huduma kwa njia ya ubia unatoa matumaini ya kukidhi mahitaji ya huduma za matengenezo kwa aina mbalimbali za magari na mitambo."

Niendelee kuzishauri wizara kushirikisha sekta binafsi katika miradi na programu mbalimbali za kimaendeleo ili kuharakisha maendeleo ya wananchi. Kwa kufanya hivyo, tutawatendea haki wananchi ambao kiu yao ni maendeleo.


*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o
KLINIKI YA FIKRA
Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

WEWORK CONSULT

# Fanya haya kupata maendeleo binafsi



Dhana ya Maendeleo Binafsi (Personal Development) inahusisha mchakato wa wewe mtu binafsi kuboresha maisha yako kwa njia mbalimbali ili kufikia uwezo wako kamili, iwe kwa upande wa kitaaluma, kibinafsi, au kihisia.

Dhana hii inalenga kuongeza maarifa, ustadi, uwezo, na ufahamu wako wa mambo ili uweze kuishi maisha yenye maana zaidi na yenye mafanikio. Kama unataka kuendelea ni muhimu sana uzingatie mambo yafuatayo kwenye maisha yako. Bila mambo haya yanayoelezewa hapa chini, usifikirie kabisa dhana ya maendeleo yako binafsi. Vipengele hivyo vya ukuaji binafsi ni kama ifuatavyo:-

1. Kujiwekea malengo – Mpango wa maendeleo yako unaanza na hatua ya kubaini unachotaka kufanikisha katika maeneo tofauti ya maisha yako, kama kazi, mahusiano, afya au kipato. Watu wengi wanafanya kazi, wanasoma au kutekeleza majukumu bila kujua wanatamani kufikia hatua gani mwisho. Bila kuona hatma na unacholenga, huwezi kuzalisha nguvu (energy) kukufikisha unapopahitaji.
2. Kujitambua – Hatua ya pili kuelekea maendeleo yako ni kuelewa nguvu zako, udhaifu wako, thamani zako, na nini kinakupa motisha. Kujitambua kinakupa uelewa wa maeneo ya kuweka nguvu kubwa na maeneo ya kuyapunguza ndani yako. Hivyo unaelekeza nguvu nyingi kwenye eneo ambalo una nguvu nalo zaidi. Hii inakupa msingi wa kufanya maamuzi bora.
3. Kujifunza – Hatua ya tatu ya maendeleo yako ni kuweka jitihada za kujifunza ujuzi mpya au maarifa kwa njia ya masomo rasmi au isiyo rasmi ili kujiendeleza. Ni muhimu kujifunza kila kitu na kisha kujifunza kwa undani kwenye mambo ambayo yanaendana na nguvu zako na malengo yako ya msingi.
4. Kujiendeleza kihisia (Emotional Development) – Hatua nyingine muhimu na ambayo watu wengi hawafanyi ni kuweka juhudi katika kuboresha jinsi unavyoshughulika na hisia zako, yaani kuwa na udhibiti bora wa hisia, na kuelewa hisia za wengine (empathy). Ni muhimu sana kushughulika na hisia zako.
5. Kujenga nidhamu – Hatua nyingine muhimu sana kwenye hatua za maendeleo yako ni kuweka na kufuata ratiba au mazoea ambayo yatakusaidia kuboresha utendaji wako wa kila siku. Acha kabisa kutenda kwa mazoea. Jenga ratiba ya mambo yako ya msingi, yape nafasi na jenga nidhamu kubwa ya kutekeleza mambo yako kwa ratiba.
6. Afya ya mwili na akili – Pamoja na hatua hizo, ni muhimu sana kuipa kipaumbele afya yako kwa njia ya mazoezi, lishe bora, na kutunza afya ya akili kwa njia ya mindfulness au kupunguza msongo wa mawazo. Hii itakupa uwezo wa kusimamia malengo yako kikamilifu sababu afya yako ya mwili na akili vinakuwa vizuri na utulivu.

Pamoja na hayo, unapozingatia suala zima la maendeleo binafsi kwa ajili yako, ni muhimu kutambua mambo yafuatayo:-

- Ni mchakato endelevu: Maendeleo binafsi si jambo la mara moja bali ni mchakato unaoendelea. Hakuna maendeleo yaliyosimama, ni ama unaendelea au unarudi nyuma. Siku utakayoacha mchakato wa kutekeleza malengo yako halisi ya ukuaji, ndiyo siku utakayoanza kushuka kimaendeleo. Kutokana na ukweli huu, ni muhimu kujitathmini mara kwa mara na kufanya marekebisho inapobidi.
- Ni muhimu kuweka malengo yanayopimika: Ili maendeleo binafsi yawe na maana, malengo yanayowekwa yanapaswa kuwa mahususi, yanayopimika, yanayoweza kufikiwa, yanayohusiana na maisha yako, na yenye kipimo cha muda (SMART goals).
- Ni muhimu kuzingatia uboreshaji wa ustadi: Kujitolea muda kujifunza au kuboresha ustadi na tabia zinazohitajika kwa ajili ya kufanikisha malengo hayo ni suala la msingi mno. Mambo yanabadilika kila siku ni muhimu kujifunza mambo mapya na kufanya maboresho kwenye ustadi wako
- Ni muhimu kuzingatia msaada wa nje: Mara nyingi, watu wanafanikiwa zaidi wanapopata msaada kutoka kwa wengine kama vile walimu, wafanyakazi wenza, au hata makocha wa maisha (life coaches). Kuna watu wengi wanaamini kwenye kazi zao wenyewe na mipango pekee. Hawa wanachelewa sana kuendelea. Siku zote inua macho, angalia msaada, angalia mbinu mpya, angalia washauri wazuri angalia watu wanaoweza kukuonesha changamoto kwako na kukushauri, tafuta mentors, tafuta vipaji vya kukusaidia, nk. Utaendelea vizuri na kwa haraka.

Dhana hii inalenga kubadilisha maisha ya mtu ili aweze kuwa toleo bora zaidi la nafsi yake, kwa kuleta mabadiliko chanya kwenye nyanja mbalimbali za maisha.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa taasisi, kikundi, kanisa, umoja, NGO au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

Wework Consult
Your Partner in Growth.

# Utata wa kifo cha John F Kennedy wa Marekani-5



LEE HARVEY OSWALD

**Simulizi kuhusu utata wa kifo cha Rais wa 35 wa Marekani John Fitzgerald Kennedy aliyeingia ofisini Januari 20, 1961 hadi alipouawa Novemba 22 mwaka 1963. Ikiwa ni miaka 61 imepita tangu kifo hicho, tumeangalia safari yake ya kutembelea Jimbo la Texas akiwa na malengo kadhaa, kubwa likiwa ni kujiimarisha kisiasa katika jimbo hilo baada ya kutofanya vizuri sana katika uchaguzi uliokuwa umemwingiza madarakani. tulianza kuangalia namna safari yake ilivyotangazwa, maofisa usalama walivyokagua maeneo ya kupita, safari ilipoanza kwa njia ya gari kutoka Kiwanja cha Ndege cha Love Field kuelekea Dallas Trade Mart, katikati mwa jiji la Dallas, Jimbi la Texas pamoja na mpangilio wa magari ulivyokuwa. Wiki iliyopita tuliagalia jinsi alivyopigwa risasi, akakambizwa hospitali na kisha makamu wake, Lyndon Johnson akawa anatakiwa kutangaza rasmi kifo chake ili kuondoa utata. Mwandishi Wetu, HAMID YASSIN anaendelea kuangalia kilichojiri baada ya kupigwa risasi.**

Gavana wa Jimbo hilo la Texas kulikotokea mauaji, John Connally ambaye alikuwa gari moja na Rais Kennedy anaeleza kuwa, baada ya hapo akawa anaanza kugeuka na ndipo ambapo alisikia maumivu kifuani na alihisi kuwa amepigwa risasi ambayo hata hakuisikia mlio wake.

Maelezo yake yanathibitishwa na ukiangalia kipande cha video, Connally anaonekana akitunisha mashavu kama anapuliza hewa nje na kukunja uso kwa uchungu katika frame ya 275 kuonyesha kwamba risasi ilikuwa imempata muda huo.

## UTATA

Sasa, kwa nini nasisitiza na kuonesha vidhibiti kuwa risasi iliyompata Kennedy katika frame ya 224 haikumpata Connally? ni kwamba, serikali ya Marekani kupitia Warren Commission wamekuwa wakieleza kuwa risasi iliyompata Kennedy ndiyo hiyo hiyo ilitokeza kifuani kwake na kwenda kumpiga Connally.

Ili hoja hii iwe sahihi maana yake ni kwamba kwa kuzingatia kasi ya mwendo wa risasi, tukio hili (risasi moja kumpiga Kennedy na Connally) lingetokea ndani ya 1/100 ya sekunde (sekunde moja gawanya kwa mia moja). Na tukio linalotokea ndani ya 1/100 ya sekunde haliwezi kurekodiwa kwenye 'frames' tofauti ni lazima litatokea kwenye 'frame' moja ya video.

Kutoka 'frame' namba 224 ambayo Kennedy anapigwa risasi mpaka 'frame' namba 275 ambayo Connally anaonyesha kuanza kuugulia maumivu ni takribani tafauti ya theluthi ya sekunde.

Theluthi ya sekunde ni muda mwingi sana kwa risasi moja kusafiri kutoka kwa Kennedy kumpata Connally.

Maelezo pekee ya kuelezea hili ni kwamba risasi ya kwanza kumpata Kennedy haikumpata Connally. Zilikuwa risasi mbili tofauti.

Lakini pia theluthi ya sekunde haitoshi kufyatua risasi mbili kutoka katika bunduki aina ya Mannlicher Carcona.

Ukipiga risasi unahitaji kusubiri sekunde kadhaa ili 'kuikoki' tena bunduki na uweze kupiga tena, kwa kifupi ni kwamba kwa namna yoyote ile au muujiza wowote ule haiwezekani kufyatua risasi mbili ndani ya theluthi ya sekunde kutoka katika bunduki ya aina hii.

Kwa hiyo hii inatueleza kwamba risasi iliyompiga Kennedy na iliyompiga Connally zilikuwa risasi mbili tofauti na zilipigwa kutoka kwa watu wawili tofauti.

## SWALI NI KINA NANI WATU HAWA?

Kabla hatujafika mbali kuanza kujiuliza ni nani mwingine labda alifyatua risasi nyingine hebu tuangalie vidhibiti zaidi.

Baraza la Senate liliwahi kuunda kamati ya kuchunguza mauaji mbalimbali ya kupangwa yaliyowahi kutokea nchini Marekani. Kamati hii iliitwa 'House Select Committee on Assassinations' au kuwa kifupi kama (HSCA).

Moja wapo ya chunguzi walizofanya ni kuhusu mauaji ya Rais Kennedy.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo alikuwa ni mtaalamu nguli wa patholojia, Dr. Cyril Wecht.

Dr. Wecht aliandika andiko la maoni yake kwa kamati hii teule ya Senate na akawaeleza kuhusu nadharia aliyokuja nayo kuhusu tukio hilo ambayo nadharia hii ilikuja kujulikana kwa wengi kama "Right to Left trajectory."

Kama nilivyoeleza kwamba, Serikali kupitia Warren Commission wanadai kuwa risasi zilipigwa na Lee Harvey Oswald akiwa mkono wa kulia wa jengo la Texas School Books Depository.

Katika andiko lake kwenda kwa HSCA, Dk. Wecht anaeleza kwamba, kwa kuzingatia kuwa ripoti ya serikali inaeleza kuwa risasi ilifyatuliwa kutoka ghorofa ya sita kutoka kwenye jengo tajwa, na pia kuzingatia upande wa jengo ambao unaelezwa Oswald alikaa, kwa maoni yake haiwezekani kwa risasi hiyo iliyompata Kennedy upande wa kulia pia kumpata Connally upande wa kulia wa ubavu chini kidogo ya kwapa.

## KWA NINI?

Ukipima pembe mlalo (horizontal angle) kutoka jengo la Texas School Books Depository kwenda kwenye gari aliyokuwamo rais na mahali ilipokuwa katika 'frame' 190 ya kipande cha video unapata nyuzi 13 (kutoka kushoto kwenda kulia).

Papo hapo pia ukipima pembe wima (vertical angle) kutoka ghorofa ya sita kwenda kwenye gari ya Rais unapata nyuzi 21 kama utapima kwa kuchukulia kuwa barabara ilikuwa tambarare iliyo sawa (horizontal plane) lakini kama ukizingatia kuwa gari la rais lilikuwa linapita kwenye barabara yenye 'slope' ya nyuzi 3 maana yake kwamba pembe wima ya kutoka ghorofa ya sita mpaka kwenye gari ya Rais inakuwa ni nyuzi 18.

## UHUSIKA WA LEE HARVEY OSWALD*

Baada ya kushambuliwa kwa msafara wa Raid Kennedy na hatimaye kupelekea kifo chake, mara moja ndani ya saa chache akakamatwa mtu anayejulikana kama Lee Harvey Oswald na kushutumiwa kuhusika na tukio hili.

Hii ilikiwaje? Nitaeleza kile ambacho serikali ya Marekani wanajaribu ulimwengu wote waamini.

Marion Baker ni afisa polisi wa eneo la Dallas na siku ya tukio alikuwa amepangiwa simu kuwa moja ya wasindikiza msafara kwa pikipiki.

Pikipiki yake ya polisi ilipangwa nyuma ya magari waliyopanda waandishi wa habari kama ambavyo nilielezea mpangilio wa msafara katika sehemu ya pili ya makala hii.

Baker anaeleza kwamba siku hiyo ya tukio, akiwa kwenye msafara sekunde chache baada ya kukata kona kutoka Huston Street na kuingia Elm Street msafara ulipotembea umbali wa kati ya futi 60 au 80 alisikia mlio mkubwa wa risasi. Baker anadai kwamba kwa uzoefu wake aligundua kuwa mlio huo ni wa 'Rifle' yenye nguvu kubwa na kuzingatia mlio uliotoka alihisi kwamba bunduki hiyo imefyatuliwa kutoka eidha Jengo la mbele yake (Texas School Book Depository) au jengo lililo mkabala na jengo hili kwa upande wa kulia, yaani jengo la Dallas Textile Building (DalTex).

Baker anaeleza kwamba, alipoangalia kwa umakini zaidi katika jengo la Texas School Books Depository akaona njiwa waliokuwa juu ya jengo wanaruka na kutawanyika kutoka kwenye paa.

Baker anaeleza kwamba moja kwa moja akaendendesha pikipiki yake mpaka kwenye kona ya Huston Street na Elm Street ambako alipaki pikipiki yake na kisha kuelekea kwenye jengo la Texas School Books Depository na kuingia ndani ambako alikutana na msimamzi wa jengo hilo Bw. Roy Truly.

Moja kwa moja baada ya kumueleza kwa haraka haraka kuhusu kilichokuwa kinaendelea huko barabarani alikotoka na kwa nini yuko hapa, yeye na Roy wakapanda mpaka ghorofa ya kwanza na kuanza kupiga kelele mtu yeyeto aliyepo juu ashushe lifti kuja chini.

Miaka hiyo lifti nyingi hazikuwa na mfumo kama huu wa sasa ambapo unabofya kitufe na lifti inakufuata ghorofa ulilopo. Kipindi hicho ilikuwa inabidi mtu aliyepo ghorofa ambalo ndipo lifti ilikuwepo kwa muda huo airuhusu kushuka chini au kwenda juu kulingana na uhitaji wa huo.

Baada ya Baker na Roy kuita kwa sekunde kadhaa bila majibu wakaamua watumie ngazi za kawaida za jengo kwenda juu.

Wakapanda mpaka ghorofa ya pili ambako wakiwa wanaelekea kupanda ngazi kwenda ghorofa ya juu zaidi, Baker anadai kwamba alisikia mjongeo kwenye chumba kilichopo karibu yao. Chumba hiki kilikuwa kinatumika kama chumba cha chakula na wafanyakazi kwenye jengo hili.

Baker akachomoa bastola yake kutoka kiunoni na kufungua chumba hiki. Ndani ya chumba hiki walimkuta Lee Oswald.

Wanaeleza kuwa Oswald hakuonekana kuwa mtu mwenye mashaka au 'kupaniki' ila tu alishtuka kuona Polisi amemmnyooshea bastola.

Inaelezwa kuwa Oswald alikuwa anaonesha dalili zote za mtu ambaye hakuwa anajua ni nini kilikuwa kinaendelea.

Msimamizi wa jengo alimtambulisha Oswald kwa askari kuwa alikuwa ni mfanyakazi wa jengo hilo, hivyo ikambidi polisi amuache Oswald na kuendelea na upekuzi katika floor za juu.

Purukushani yote hii kutoka muda ambao Baker alisikia mlio wa risasi akiwa kwenye msafara wa Rais mpaka kuja kukutana na Oswald ghorofa ya pili ya jengo la Texas School Books Depository, ilichukua kama sekunde 74 mpaka sekunde 90 tu.

*Itaendelea*

# Ukraine kutangaza mpango wake wa ushindi wiki hii

> **Ni wazi, sasa kuna sababu moja tu ya tukio hili - ni uwasilishaji kwa umma wa mpango wa ushindi.”**



**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukraine Vladimir Zelensky, amesema atawasilisha mpango wake wa ushindi wiki hii.

Kiongozi huyo wa Ukraine pia amezungumzia kuhusu mpango wake wakati wa ziara ya Marekani na Ulaya, lakini maelezo yake bado hayajatangazwa hadharani.

“Wiki hii tutawasilisha kwa washirika wote barani Ulaya mkakati wetu wa kulazimisha Urusi kumaliza vita hivi. Bila shaka, mpango wa ushindi utawasilishwa hadharani,” Ukrayinska Pravda anamnukuu Zelensky akisema.

Mapema juzi Jumatatu, Mshauri Mkuu katika Ofisi ya Rais Zelensky, Sergei Leshchenko, alisema kuwa le Zelensky atazungumzia suala hilo.

“Ni wazi, sasa kuna sababu moja tu ya tukio hili - ni uwasilishaji kwa umma wa mpango wa ushindi,” Leshchenko alisema.

Vyanzo vya gazeti la Ukraine la Ukrayinska Pravda vilithibitisha kwamba Zelensky anaweza kuwasilisha mpango wa ushindi kwa wabunge.

Mwakilishi Mkuu wa Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Kigeni, Josep Borrell, pia alitangaza uwasilishaji wa Zelensky wa mpango wake wa ushindi katika mkutano wa Baraza la Ulaya, limeandika Shirika la Habari la Ukraine la Interfax.

Mkutano wa Baraza la Ulaya katika ngazi ya wakuu wa nchi na serikali, umepangwa kufanyika kesho na keshokutwa. BBC.

## Shambulio la anga laua 21, wanane wajeruhiwa

**BEIRUT, Lebanon**

TAKRIBAN watu 21 wameuawa na wengine wanane kujeruhiwa katika shambulio la nadra la anga la Israel Kaskazini mwa Lebanon, Wizara ya Afya ya Lebanon imesema.

Shambulizi hilo lililenga jengo la makazi katika kijiji cha Aitou, chenye wakazi wengi wa Kikristo mbali na maeneo ambayo jeshi la Israel limekuwa likifanya mashambulizi mengi dhidi ya kundi la wapiganaji wa Kiislamu la Kishia la Hezbollah.




Wakazi walisema kuwa familia iliyohamishwa hivi majuzi na vita imekuwa ikiishi huko.

Jeshi la Israel halikutoa maoni yake mara moja kuhusu ripoti hizo. Lakini shambulizi hilo lilikuja baada ya waziri mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu kuapa “kuendelea kuishambulia Hezbollah bila huruma kila mahali nchini Lebanon - ikiwa ni pamoja na Beirut”.

“Kila kitu kinafanyika kwa umakini na kwa muda uliopangwa.Tumethibitisha hili hivi majuzi na tutaendelea kulithibitisha katika siku zijazo pia,” aliongeza.

Alikuwa akizungumza katika ziara yake katika kambi ya kijeshi kaskazini mwa Israel ambapo ndege isiyo na rubani iliyorushwa na kundi linaloungwa mkono na Iran iliwaua wanajeshi wanne wa Israel na kuwajeruhi makumi ya watu siku ya Jumapili usiku.

Jeshi lilisema linachunguza jinsi ndege hiyo isiyo na rubani ilivyokwepa mifumo yake ya kisasa ya ulinzi wa anga na kupiga kituo cha mafunzo cha Golani Brigade kilichopo karibu na mji wa Binyamina. BBC.



## WHO yaidhinisha chanjo mpya ya mpox kwa vijana

**GENEVA, Uswisi**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeidhinisha chanjo mpya ya mpox Bava.Co kwa vijana wenye umri wa miaka 12 hadi 17.

Kundi la vijana, limetajwa kuwa katika hatari kubwa ya milipuko ya ugonjwa huo ambao umezua wasiwasi duniani.

WHO ilisema katika taarifa yake kwamba ilitoa kibali cha awali cha chanjo hiyo ya Jynneos kwa vijana Oktoba 8, mwaka huu.

WHO ilitangaza mpox kuwa dharura ya afya ya umma duniani kwa mara ya pili ndani ya miaka miwili Agosti, mwaka huu baada ya aina mpya ya virusi kuenea kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hadi nchi jirani.

VOA.

## 12 wafa, 33 wajeruhiwa ajali ya basi

**CAIRO, Misri**

WATU 12 wamefariki dunia na wengine 33 wamejeruhiwa katika ajali ya basi kwenye barabara kuu nchini Misri.

Wizara ya Afya ya nchi hiyo ilisema katika taarifa yake kuwa ajali hiyo ilitokea juzi Jumatatu ambapo basi hilo liliwabeba wanafunzi waliokuwa wakirudi nyumbani kutoka Chuo Kikuu cha Galala Jimbo la Suez Mashariki mwa Misri, wakati

Gazeti linalomilikiwa na serikali la Akhbar al-Youm, liliripoti kuwa hapakuwa na gari lingine lililohusika katika ajali hiyo na kwamba uchunguzi umeanzishwa kubaini kasi ya basi hilo na mazingira ya ajali hiyo.

Wizara ya Afya ilisema waliojeruhiwa walipelekwa katika hospitali ya karibu, 19 kati yao waliondoka hospitali juzi Jumatatu jioni.

Ajali za barabarani ni jambo la kawaida nchini Misri, ambako madereva mara nyingi hupuuza sheria za usafiri wa barabarani na barabara nyingi ziko katika hali mbaya.

Barabara ya Galala ambako ajali hiyo ilitokea, hata hivyo, ni moja ya maelfu ya kilomita ya barabara kuu na njia za juu zilizojengwa katika mwongo mmoja uliopita, kama sehemu ya kipaumbele cha serikali katika miradi ya miundombinu.

Takwimu rasmi zinasema zaidi ya watu 5,600 waliuawa katika ajali za barabarani mwaka 2023 katika taifa hilo lenye idadi ya kubwa zaidi ya watu katika mataifa ya Kiarabu.VOA.



## 200 mbaroni wakiandamana kupinga vita vya Gaza

**NEW YORK, Marekani**

TAKRIBAN waandamanaji 200 waliokuwa wakipinga vita vya Israel huko Gaza juzi Jumatatu, walikamatwa wakiwa wameketi nje ya jengo la biashara kuu za hisa mjini New York.

Waandamanaji hao, wakiwa nje ya jengo hilo maarufu lililopo kwenye Kitongoji cha Manhattan, walisikika wakisema kuwa “Let Gaza Live” Up up with liberation, down down with occupation,” ambazo ni kauli za kutetea uhuru wa wakazi wa Gaza na kupinga mashambulizi yanayoendelea kutekelezwa na Israel.

Beth Miller ambaye ni mwanaharakati wa kisiasa kwenye kundi la Jewish Voice for Peace, ambalo liliitisha maandamano hayo, alisema: “Sababu yetu kukusanyika hapa ni kuomba Marekani isite kutuma mabomu kwa Israel, na ikome kufaidi kutokana na mauaji ya halaiki Wapalestina yanayotekelezwa na Israel.”

Wakati huo huo, kundi ndogo la waandamanaji wakiwa na vibendera vya Israel, walionekana karibu na kundi hilo lililokuwa likipinga Israel.

Kwenye ripoti tofauti, Shirika la Msalaba Mwekundu la Lebanon lilisema juzi Jumatatu kwamba shambulizi la anga la Israel, liligonga jengo la makazi

VOA.

# UV-CCM imuenzi Maneti kwa kuifufua Vijana Jazz



Marehemu Hemed Maneti

**Na Hamid Yassin**

IMETIMU miaka 34 tangu kifo cha mwanamuziki nguli wa bendi ya Vijana Jazz Hemed Maneti Ulaya 'Chiriku' kilichokea siku ya Alhamisi jioni Mei 31 mwaka 1990.

Ndiyo, kuna kila sababu ya kumkumbuka marehemu Maneti kutokana na umahiri wake kimuziki na jinsi alivyoipigania bendi hiyo ya Vijana Jazz enzi zake ambayo kwa sasa ni kama 'ipo haipo' huku ikizidi kufutika kwenye ulimwengu wa muziki hapa nchini.

Kama kuna wimbo uliomtoa mwanamuziki Maneti mara baada ya kujiunga na Vijana Jazz, basi wimbo huo ni ule wa 'Niliruka ukuta' uliopigwa kwenye miaka ya themanini.

Maneti, maarufu kama "Chiriku wa Tanzania" au ukipenda muite 'Simba Mwenda kimya' aliiroga jamii nzima kwa wimbo huo ambao ulisimulia kisa kilichowagusa wengi.

Mashabiki, vijana kwa wazee, waliupenda wimbo huo kiasi cha kuwa dira ya kuacha ufuska na hasa kuvamia wake za watu.

Maneti katika wimbo huo anamlaumu mwanadada mmoja aliyemdanganya kuwa hakuwa na mume wala tegemezi lolote la mwanaume wakati haikuwa kweli.

Binti huyo alimhakikishia Maneti (katika tungo) kwamba, hata chumba alichokuwa amemkaribisha 'kupumzika' naye kilikuwa chake na alikuwa amepanga mwenyewe na kukilipia kodi.

Lakini, kama ilivyo siku zote kuwa za mwizi ni arobaini, ndivyo ilivyokuwa kwa mwanadada huyo. Kwani ilipofika saa nane za usiku siku hiyo, Maneti alistuka kusikia mlango ukigongwa kuashiria mwenye nyumba karejea kwake.

Akiwa hana hili wala lile, ghafla akili zilimtuma ajiokoe kwa kuruka ukuta na Mungu mweza wa yote, akafanikiwa na kulikwepa fumanizi la mwaka ambalo pengine lingemsababishia kifo hata kabla ya muda wake.

Kwa hakika hiyo ilikuwa ni hatari kubwa. Kwani wengi wanapoteza maisha yao kwa ufuska wa nje ya ndoa na hasa kufakamia wake za watu ambao mara nyingi baadhi yao hawasemi ukweli halisi wa haiba zao katika ndoa.

Basi, 'kijana' Maneti kwa wakati huo akabaki kulalamika tu juu ya kitendo cha yule mwanadada na hapo akamtuma shogaye kwenda kumueleza kuwa vitendo vya aina ile si vizuri.

"Na ukifika mwambie ajirekebishe. Mambo kama yale mabaya na yana hatari. Nimeponea chupuchupu sababu ya yeye. Kama si kuruka ukuta ingekuwa hatari," hayo ni baadhi ya maneno kwenye wimbo huo ambao unaonesha ni jinsi gani mwanamuziki huyo alivyokuwa na hisia kali za utunzi ambazo zinaonesha jinsi mtu alivyoepuka kifo kwa tundu la sindano.

Leo hii, ukimuuliza mjuzi wa masuala ya tunzi za nyimbo atakwambia kuwa Maneti hakuwa mtu wa kawaida katika fani hiyo.

Kwani mara zote alikuwa mbunifu hasa kwenye kutunga mitindo ya vibwagizo vya bendi ya Vijana.

Alianza na mtindo wa 'Hekaheka' kwa maana kwamba alikuwa ni kijana aliyekuwa kwenye harakati za kutafuta maisha. Hapa ni wakati alipotoka Cuban Marimba kwenye miaka ya mwishoni mwa sabini kwa kushawishiwa na Hamza Kalala "Komandoo wa Muziki" ambaye pamoja na kina-John Ondolo Chacha walikabidhiwa bendi ya Vijana na Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kuiendesha.

Komandoo Kalala aligundua haraka kuwa ili kuipaisha bendi hiyo ilikuwa hapana budi kupata vipaji vya mfano wa Maneti aliyekuwa mjini Morogoro na bendi hiyo ya Cuban Marimba baada ya kifo cha muasisi wake, Salum Abdallah.

Baadaye Maneti akabuni tena mtindo wa 'Kokakoka' ukiwa na maana kuwa baada ya kuhangaika sasa alikuwa amewasha jiko la mkaa na kuanza kuukoka moto ili ukolee vyema.

Katika kipindi hicho nyimbo kadhaa zilitungwa kushajiisha mtindo huo.

Ndipo ilipokuja 'baba lao' kwenye mwaka 1986 alipo utangazia ulimwengu wa wapenda muziki kuwa moto aliokuwa ameuwasha sasa ulikuwa umepamba na kuwaka barabara tayari kuivisha chungu chochote kile hata kama ni cha chuma.

Ndipo alipoweka wazi mtindo huo kwa kuuita 'Pambamoto'. Mtindo huu ulikolea. Haukumuacha mtu. Tangu watoto hadi wazee walikuwa wanaujua na kuukubali kupita maelezo.

Baadhi ya nyimbo zilizohanikiza mtindo huo ni 'Mary Maria', 'Wifi Zangu', 'Shingo feni', 'Mwisho wa mwezi', 'Bujumbura', 'Ilikuwa Lifti', 'Tambiko la Pambamoto' na nyingine kadhaa.

Kana kwamba ilikuwa ni kuweka petroli kwenye moto, uongozi wa UVCCM ulimkubalia Maneti na mwenzake Komandoo Kalala kufanya marekebisho ya bendi.

Ndipo hapo wakajumuishwa kina Eddy Sheggy, Rashid Pembe, Adam Bakari maarufu "Sauti ya Zege", Mohammed Gotagota, Juma Choka na wengine kadhaa.

Hadi hapo, habari jijini Dar na Tanzania nzima ilikuwa ni "Maneti na Vijana Orchestra" tu. Ndiyo; Vijana Orchestra tu.

Ililazimika kubadilishwa jina kutoka Vijana Jazz hadi kuwa Vijana Orchestra kutokana na mseto wa wanamuziki mahiri vijana na waliobobea waliokuwemo kwenye bendi hiyo kwa wakati huo.

Kuanzia hapo ukumbi wa starehe wa Vijana uliokuwa Kinondoni, utakuwa shahidi wa nyota ya mtukuka huyo kimuziki hapa nchini.

Kwani pamoja na ukubwa wa ukumbi huo, watu walifurika kupita maelezo na hivyo kufanya fukwe za Rungwe Oceanic, Silver Sands, Bahari Beach na Africana Hotel kupoteza mashabiki.

Wote walijichimbia kwenye ukumbi huo wa Vijana kuona muziki wa Kitanzania ukipigwa na vijana wa Kitanzania waliokuwa mahiri katika fani hiyo.

Ilikuwa wakati huo, Maneti alipoongeza madoido ya mtindo wake mpya na kuuita "Pambamoto Awamu ya Pili".

Kana kwamba hiyo ilikuwa 'kibakuli', mara baada ya hapo Maneti alibuni tena mtindo mwingine ulioitwa "Pambamoto

Itaendelea Uk. 21.



Kikosi cha Vijana Jazz cha mwaka 1989

# UV-CCM imuenzi Maneti kwa kuifufua Vijana Jazz

**Inatoka Uk. 20.**

Awamu ya Pili Shambulia".

Wallah, ilikuwa ni shambulia kweli. Si utani wala udaku. Magitaa yalirindima kwa ustadi mkubwa chini ya uongozi wake marehemu Shabaan Yohanna maarufu "Wanted" ambaye alikuwa akichambua "nyuz-bin-nyuz" za gitaa ongozi la solo kiukweli na uhakika.

Hadi hapo, palikuwa hapatoshi kwenye ukumbi wa Vijana. Hakukuwa na sehemu ya kukanyaga wala kutema mate. Kwani ulipofanya hivyo ulikuwa unawatemea wenzako au kuwakanyaga. Ikabaki kuwa kila mtu alipokuwako basi alilazimika kubakia na kucheza akiwa papo hapo.

Kwa hakika ulikuwa wakati wa njaa kwa bendi nyingine. Hakukuwa na cha Marquiz Original wala wana-Safari Sound Orchestra kwa bendi za Kikongo na kwa njaa hiyo hiyo kwa bendi za Mlimani Park Orchestra na OTTU Jazz Band kwa bendi za Kitanzania.

Ilikuwa ni nyimbo za 'Ogopa Tapeli', 'Ngapulila', 'Wivu' na nyingine zilizokuwa moto wa kuotea mbali.

Vijana Orchestra ikawa ni Vijana Orchestra maradufu. Ukipenda basi "Pambamoto" ikawa "Pambamoto" kwelikweli. Ukichanganya na kibwagizo cha 'Shambulia' ikawa 'balaa- bin-taabu mjini'.

Bendi ikawa haishikiki, Maneti akawa hakamatiki. Kwa mantiki hiyo, "Simba huyo mwenda kimya" akawa kama yupo juu ya dunia!



**Marehemu Eddy Shaggy**

Akaroga kila aliyemuona jukwaani kutokana na sauti yake tamu, sura yake ya kuita, weupe wake wa ung'avu, meno yake meupe kama karatasi ya daftari, tambo lake maridhia lisilochusha kuliangalia na kikubwa kuliko vyote ilikuwa namna alivyokuwa akinengua kwa kuparamia nguzo zilizokuwa zikishikilia jukwaa.

Hakya Mungu, kwa muktadha huo, akawaacha mashabiki wote hoi-bin-taaban.



**Marehemu Shaban Yohana 'Wanted' (kushoto) enzi hizo akiwa na mwandishi wa makala haya**

Katikka kipindi hiki ambapo kuna haja ya kuandaa tamasha la Kumbukumbu ya Miaka 34 ya Maneti, tutaona mengi yakiandikwa na kutangazwa kuhusu 'kijana' huyu ambaye ndugu na rafiki zake wa karibu hutokwa chozi kila wasikiapo nyimbo zake ambazo kwa sasa zinarejewa upya na binti yake mahiri katika uimbaji Komweta Hemedi Maneti Ulaya ukipenda mwite "Chiriku Mtoto".

Aidha. huu ni wakati mwafaka kwa Jumuiya ya Umoja wa Vijana, UV-CCM, kuangalia upya mbinu na mikakati ya kuifufua Bendi ya Vijana Orchestra ikiwa ni njia mojawapo ya kumuenzi hayati Hemedi Maneti.

Hii ni kwa kuipa umuhimu kuiendeleza na kuwafanya wanamuziki walio hai hivi sasa na hata wengine wapya wa bendi hiyo kufanya muziki wao kama ilivyokuwa zamani enzi za uhai wa mwanamuziki mwenzao hayati Maneti.

Nadhani ni busara kubwa kwa UV-CCM na hasa CCM yenyewe kukumbuka fadhila ya wanamuziki hao ambao walifanya kazi kubwa ya uhamasishaji Chama na jumuia zake kwani walitumia vipaji vyao kuburudisha, kuelimisha, kuhabarisha na kuonya jamii masuala mbalimbali ya siasa, jamii na uchumi.

Sina shaka na uongozi wa CCM Awamu ya Sita ambapo ina viongozi mahiri na vijana wachapa kazi chini ya Mwenyekiti wao Dk.Samia Suluhu Hassan.

Naamini kabisa atakisikia kilio hiki na kutoa sapoti kubwa na msukumo kwa UV-CCM Taifa chini ya Mwenyekiti wake wa sasa, Jemedari Mohamedi Kawaida kuweza kusukuma uwezeshaji wa kuifufua Vijana Orchestra kurejea jukwaani.

Kwani ni aibu kwa Jumuiya makini kama hii ya UV- CCM kushindwa kuiendesha bendi ambayo ni moja ya Idara nyeti ya uhamasishaji ndani ya CCM hasa kwa wakati huu wa kuelekea chaguzi za Serikali za Mitaa Novemba 27 na ule Uchaguzi Mkuu wa Taifa mwakani 2025.

Naamini pia kuwa Katibu Mwenezi wa CCM Taifa, Amosi Makalla ni kijana msomi mchapakazi ambapo kwa sasa yupo ziarani mikoa mbalimbali hapa nchini akitekeleza majukumu aliyopewa na Chama chake.

Anaendelea kufanya mabadiliko makubwa ndani ya Chama na nje ya Chama. Bila shaka atakubaliana na mimi kuwa wakati umefika kila mmoja kwa nafasi yake achape kazi kwa vitendo na hili linanisukuma kusema upo umuhimu wa kuirejesha Vijana Orchestra ili wanamuziki wake warejee kazini na kulijenga Taifa.

Pia naamini Mohamed Kawaida ana uwezo wa kuwaondoa shaka wanamuziki wa bendi hii (kama bado wapo pamoja) hasa kutokana na kwamba tangu kupewa nafasi hiyo amekuwa moto wa kuotea mbali katika kuimarisha Jumuia ngazi zote.

Kwa hiyo namkumbusha Mwenyekiti Kawaida kuwa hii iwe ni 'Amsha amsha' ili Vijana Orchestra warudi majukwaani na waweze kuitumia fursa ya kunadi na kuhimiza 'Kazi ziendelee' kama anavyotaka Rais wetu Dk. Samia.

Naamini kwa kufufua bendi hiyo inatosha kumuenzi hayati Hemedi Maneti kama alivyoahidi aliyekuwa Katibu Mkuu wa Jumuia hiyo wakati mwanamuziki huyo akizikwa kwao Muheza mkoani Tanga, marehemu Mohammed Seif Khatib kuwa UV-CCM itafanya kila linalowezekana kumuenzi hayati Maneti kwa kazi kubwa aliyoifanya hapa nchini.

**Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.**



**Marehemu Jery Neshoni 'Dudumizi' (kushoto) na kulia ni Benovilla Anthony enzi hizo wakiwa na mwandishi wa makala haya**

# Hakuna tunachomdai Mbwana Samatta

## ● Amewatoa kimasomaso Wanambagala

**Na Hamid Yassin**

UNAUKUMBUKA ule wimbo wa Diamond Plutinum wa 'Kwetu Mbagala'? Ulikuwa na kisa cha kusisimua ingawa wapo wengi walisikitishwa na mashairi yake.

Mwanamume aliyevaa uhusika katika wimbo huo anasikitika kukataliwa na mlimbwende mmoja huku akihisi eti kwa sababu tu anaishi Mbagala! Yaani Mbagala ni mahali wanaishi watu wa hadhi ya chini. "Hapa nyumba pale jalala!"

Huko Mbagala kunakodharauliwa na wengi ndiko kumemtoa mfalme wa soka wa muda wote hapa nchini, si mwingine bali ni Mbwana Ally Samatta.

Yamesemwa mengi mabaya juu ya Samatta kiasi cha mwenyewe kuchukua maamuzi ya kustaafu kuchezea timu ya taifa, lakini kwa busara ya viongozi wa soka nchini, baba yake mzazi, Mzee Ally Samatta na wadau wengine, hatimaye amekubali kurejea kuichezea timu hiyo.

Samatta ameichezea mechi nyingi Stars na kuifungia magoli mengi muhimu kiasi cha kuiongoza kufuza Kombe la Mataifa ya Afrika mara mbili katika miaka ya hivi karibu.

Na hivi sasa baada ya kukubali kurejea amesema azma yake ni kuhakikisha timu ya taifa, Taifa Stars inafuzu tena kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON, zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Kama nilivyosema hapo juu, Samatta ameshaifanyia mengi Tanzania, ikiwemo kuitangaza vema ndani na nje ya mipaka yetu, hivyo hakuna tunachomdai na anayofanya hivi sasa akiwa anaelekea mwishoni mwa soka lake ni bonasi tu kwa Watanzania.

Nakumbuka jinsi Mwanambagala huyu alivyotutoa kimasomaso Watanzania pale alipocheza hadi ligi kubwa kuliko zote duniani kwa sasa ya England. Kule aliichezea moja ya timu kubwa ya Aston Villa.

Kabla ya kwenda Ligi Kuu ya England (EPL), mshambuliaji huyo alitokea kwenye ligi nyingine kubwa ya Ubelgiji ambako aliichezea timu ya KRC Genkj.

Akiwa anakipiga pale KRC Genk nahodha huyu wa Tanzania aliifanyia mengi timu hiyo ikiwemo kuipatia ubingwa wa nchi hiyo baada ya kupita kipindi kirefu.

Pia akiwa Genk alifanikiwa kucheza michuano mikubwa ya Klabu Bingwa Ulaya ambapo moja ya mechi kubwa ambayo naamini itabaki kwenye kumbukumbu zake na Watanzania kwa ujumla ni ile dhidi ya miamba ya Liverpool FC.

Katika pambano lile siyo tu kwamba Samatta alicheza, bali pia alifanikiwa kufunga bao dhidi ya miamba Majogoo hao wa Anfield. Goli hilo lilikuwa likisubiriwa kwa hamu na mashabiki wa mpira wa miguu nchini Tanzania.

Hata hivyo, matokeo ya mwisho ya mchezo huo wa Klabu Bingwa Ulaya yalikuwa mabaya kwa Genk kwa kulazwa kwa goli 2-1.

Samatta, aliunganisha kwa kichwa mpira wa kona mpaka wavuni katika dakika ya 40 ya mchezo.






Mshambuliaji huyo ambaye ameweka rekodi ya kuwa Mtanzania wa kwanza kucheza michuano hiyo mikubwa zaidi ya vilabu barani Ulaya, alifanikiwa kupachika magoli mawili katika mechi nne alizocheza.

Tangu aondoke Tanzania miaka kadha iliyopita kulekea DR Congo kuichezea TP Mazembe ya Lubumbashi, Samatta amekuwa na mafanikio ya mfululizo.

Aliiongoza miamba hiyo kutwaa mataji matano ya ndani sambamba na kutwaa mataji mawili ya Klabu Bingwa Afrika. Pia walitwaa taji la Kombe la Shirikisho Afrika katika kipindi hicho alichokaa Congo.

Pamoja na mafanikio hayo ya mataji, Samatta pia alifanikiwa kuwa mchezaji bora wa Afrika kwa wachezaji wanaocheza soka la ndani ya Afrika wakati ule akiichezea TP Mazembe kwa mafanikio makubwa.

Nuru ya Samatta iliendelea kung'ara hadi Ulaya alipokwenda kucheza soka la kulipwa kwenye timu ya KRC Genk ya Ubelgiji.

Aliikuta timu hiyo imekaa miaka zaidi ya mitano bila taji la Ligi yao Kuu, lakini katika msimu wake wa pili tu aliiongoza kutwaa taji sambamba na kuongoza kwa magoli kwenye timu yake huku akishika nafasi ya pili kwa ligi nzima kwa kupachika magoli 24.

Alipotoka Ubelgiji kituo kilichofuata kilikuwa nchini Uturuki ambako alikwenda kujiunga na timu ya Fenerbahce baadaye akarudi Ubelgiji na kuichezea miamba ya Antwerp.

Kwa sasa Samatta yupo anacheza soka la kulipwa nchini Ugiriki katika klabu ya Paok.

Kwa huku nyumbani Tanzania nako mambo yake si haba; tangu amekabidhiwa unahodha wa timu ya Taifa toka kwa Nadir Haroub 'Canavaro', ameiongoza vema taifa hili kiasi hata cha kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) kule Misri mwaka 2019 ambapo ilikuwa mara ya pili baada ya miaka 39 kupita tangu Tanzania ishiriki michuano hiyo mwaka 1980 kule Lagos Nigeria.

Mapema Januari mwaka huu pia Samatta aliongoza Taifa Stars kwenye fainali za mashindano haya makubwa ya Afrika ya AFCON 2023.

Chini yake pia tayari Tanzania ilifanikiwa kutinga hatua ya makundi ya kuwania kucheza fainali za Kombe la Dunia kule Qatar mwaka 2022.

Huyo ndiye kijana Mbwana Samatta staa mkubwa aliyevuna fedha nyingi kutokana na mpira, lakini anayeishi maisha yasio na mbwembwe wala majivuno.

Katika kudhihiri Samatta si mtu wa kupenda makuu, alifunga ndoa kimya kimya hapa Dar yote ni katika kuepuka vurugu za mitandaoni na mitaani kutokana na jina lake kubwa alilojijenga hapa Tanzania.

Narudia hakuna tunachomdai Samatta, tumwache amalizie soka lake kwa amani na utulivu kama ambavyo mwenyewe anavyopenda kuishi.

Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.



# Baadhi ya istilahi za Kiswahili katika mpira wa miguu

Na Richard Mtambi



Mtangazaji wa soka wa TBC, Enock Bwigane



Mtangazaji wa soka wa Azam Tv, Baraka Mpenja

MAKALA haya yanajadili baadhi ya istilahi za Kiswahili zinazopaswa kutumiwa katika uga wa mpira wa miguu. Lengo ni kuonyesha kwamba Kiswahili kina istilahi za kutosha zinazokidhi mahitaji ya lugha ya mpira wa miguu, japo kwa sasa waandishi, watangazaji, wachambuzi na wapenzi wengi wa mchezo huo, wamekuwa wakitumia maneno mengi ya lugha ya Kiingereza katika uandishi, uchambuzi, utangazaji na mazungumzo yao ya kila siku.

Sababu kubwa ya kutumia istilahi za Kiingereza inawezekana ikawa ni ya kimazoea, kutokana na wapenzi wengi wa mpira wa miguu kufuatilia matangazo ya mchezo huu kupitia katika vyombo ambavyo hutumia lugha ya Kiingereza katika matangazo yao au wao wenyewe kutokujua baadhi ya maneno au istilahi za Kiswahili zinazofaa kutumika katika mchezo huu.

Kutokana na mazoea haya ya kufuatilia matangazo ya mpira wa miguu yanayotolewa na vyombo vinavyotumia lugha ya Kiingereza, wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili wamejikuta wakiathiriwa na hali hiyo.

Athari hizi zinajitokeza hata kwa watangazaji wa mpira wa miguu wa vituo vya redio na televisheni vya hapa nchini ambavyo navyo vimejikuta vikitumia istilahi za Kiingereza hata pale ambapo wanatoa matangazo yao kwa lugha ya Kiswahili.

Istilahi hizi zinazotangazwa kwa Kiingereza wakati zina visawe vyake katika Kiswahili ni nyingi mno, hata hivyo, katika makala haya tutachagua baadhi tu na hasa zile ambazo zimezoeleka sana na zinasikika mara kwa mara katika matangazo ya Kiswahili ya mpira wa miguu katika vituo vyetu vya redio na televisheni hapa nchini.

Tuanze na jina lenyewe la mchezo huu. Istilahi ya Kiingereza inayotaja mchezo huu ni football au soccer. Kiswahili kina maneno mengi ya kuueleza mchezo huu.

Hata hivyo, maneno yaliyozoeleka ni soka ambalo ni la utohozi kutoka katika lugha ya Kiingereza na maneno mengine kama vile kandanda na kabumbu.

Aidha, kuna mwongozaji au msimamizi wa mpira wa miguu kiwanjani ambaye hutumia filimbi na ishara kuongoza matendo mbalimbali ambayo wachezaji wa mpira wa miguu wanapaswa kuyafuata kwa mujibu wa sheria za mchezo huu.

Huyu kwa lugha ya Kiingereza huitwa referee. Katika Kiswahili istilahi mbili zinaweza kutumiwa unapomtaja mtu huyu, moja ni ya utohozi na nyingine si ya utohozi. Istilahi hizi ni refarii/refa na mwamuzi.

Wasaidizi wake ambao aghalabu ni wawili wanaotumia bendera wakiwa katika mistari ya pembeni mwa uwanja ambao kwa lugha ya Kiingereza huitwa assistant referees, katika lugha yetu adhimu ya Kiswahili, wanamichezo hawa huitwa waamuzi wasaidizi, ambapo unapomtaja mmoja ni mwamuzi msaidizi (assistant referee).

Vilevile, timu zinapokuwa zinapambana hujipanga katika miundo mbalimbali kulingana na malengo ya kocha au mwalimu wa timu ya mpira wa miguu (football coach) wa timu na urahisi au ugumu wa mchezo unaohusika.

Miundo hii ya uchezaji ambayo kwa lugha ya Kiingereza huitwa formation, katika lugha yetu ya Kiswahili ni mfumo/mifumo. Kuna mifumo mbalimbali ya uchezaji wa soka, mfano, nne - nne - mbili (4-4-2), tatu - tano - mbili (3-5- 2), nne - tatu - tatu (4-3-3) n.k. Mifumo hii tumekuwa tukiisikia sana ikitamkwa kwa lugha ya Kiingereza: Four - four - two, three - five - two, four - three - three n.k.

Makala haya hayakusudii kuelezea namna mifumo hii ya soka inavyochezwa, bali yanaonyesha jinsi ambavyo lugha yetu adhimu ya Kiswahili haijapitwa na jambo hili. Tunaweza kuielezea mifumo hii ya uchezaji wa soka tukaelewana vema pasi na kuhitaji matumizi ya lugha za kigeni.

Hata hivyo, imezoeleka kuwasikia watangazaji wetu wakituambia kuwa, "Leo Timu ya Dodoma Jiji inatumia formation ya four - four - two dhidi ya ile ya three - five - two inayotumiwa na KMC ya Dar es Salaam katika mchezo huu."

Kumbe wangeweza kusema tu, "Timu ya Dodoma Jiji inatumia mfumo wa nne - nne - mbili dhidi ya ule wa tatu - tano - mbili unaotumiwa na KMC."

Tunawashauri watangazaji wetu kutumia istilahi hizi za Kiswahili badala ya kung'ang'ania kutumia istilahi za Kiingereza ili lugha yetu iweze kukua zaidi, kwani moja ya njia zinazoiendeleza lugha yoyote ni ukuzaji wake wa msamiati na jinsi unavyopokewa na kutumiwa na wazungumzaji wake na hata wageni ambao wanajifunza lugha hiyo.

Vilevile, timu mbili zinapokuwa zinapambana uwanjani, licha ya kila moja kutaka kuishinda timu pinzani, pia, huzidiana katika kiwango cha kila moja kudumu kuwa na mpira.

Neno la Kiingereza possess maana yake ya Kiswahili ni miliki.

Hivyo, katika muktadha wa mpira wa miguu, kinachozungumziwa ni kumiliki mpira. Istilahi inayotumika katika Kiingereza ni ball possession, ambapo katika Kiswahili ni umiliki wa mpira.

Kiwango hiki hupimwa kwa asilimia mia moja (100%). Hivyo, iwapo timu A ikiwa na umiliki wa mpira wa asilimia 55, basi timu B itakuwa na umiliki wa mpira wa asilimia 45.

Viwango hivi vya umiliki wa mpira huonyeshwa kulingana na mchezo unaohusika na uwezo wa kukaa na mpira wa timu ambapo kunaweza kuwapo na umiliki wa mpira wa 50 kwa 50 yaani kila timu kumudu kukaa na mpira sawa na timu nyingine.

Kunaweza pia kuwapo na viwango tofauti vya umiliki wa mpira kama vile 65 kwa 35, 70 kwa 30, 80 kwa 20 n.k., kutegemea na mchezo unaohusika.

Timu ambazo huzuia kwa kiwango kikubwa katika muda mwingi wa mchezo huwa na umiliki wa mpira wa kiwango kidogo ukilinganisha na timu ambazo hushambulia.

Timu inayozuia zaidi badala ya kushambulia huitwa timu inayojihami, yaani defending team kwa Kiingereza. hata hivyo, maneno hayo ya kingereza, defending team, yanaweza kutumiwa pia kwa timu inayotetea ubingwa wake.

Kwa vile tumezungumzia kujihami, ni dhahiri kuwa timu inayojihami inapaswa kuwa na wachezaji imara katika sehemu au safu ya nyuma.

Sehemu hii ya nyuma ya timu huitwa sehemu ya ulinzi ambapo katika lugha ya Kiingereza ni defence. Mchezaji anayecheza katika nafasi hii ya ulinzi, defender kwa lugha ya wenzentu Waingereza kwa lugha yetu ya Kiswahili huitwa mlinzi.

Miongoni mwa walinzi hawa kuna mlinzi wa kati - central defender/central back na walinzi wa pembeni ambao wenzetu huwaita full backs, yaani mabeki wa pembeni, upande wa kulia na upande wa kushoto. Walinzi hawa wakisaidiana na mlinda mlango/golikipa/kipa (goal keeper) pamoja na kiungo wa ulinzi (defending midfilder) ndio wenye dhamana ya kuhakikisha kuwa goli lao linakuwa salama dhidi ya washambuliaji wa timu pinzani.

Wapinzani wanapofanya jitihada za kupata mabao huitwa timu inayoshambulia (attacking team), ambapo lengo lao huwa ni kusababisha madhara kwa walinzi wale na golikipa kwa lengo la kupata magoli na kushinda mchezo unaohusika.

Timu inayoshambulia hufanya hivyo aghalabu kwa kumtumia mshambuliaji wa kati, ambaye wengi humuita kwa Kiingereza central sricker/goal attacker, pamoja na washambuliaji wa pembeni (wingers).

**Itaendelea wiki ijayo.**

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Oktoba 16-22, 2024 |

## Victor Osimhen ajitolea kumsaidia mlemavu Nigeria

**ABUJA, Nigeri**



BAADA ya kusambaa kwa picha ya mwanamke mlemavu akiuza maji ya kunywa ya chupa katika ya mitaa ya hapa Abuja, Nigeria, kwenye mitandao ya kijamii, mshambuliaji wa kimataifa wa Nigeria, Victor Osimhen wa klabu ya Napoli ya Italia ambaye kwa sasa yupo kwa mkopo na Galatasaray, ameguswa na mwanamke huyo.

Osimhen amewasiliana na mmoja wa wanafamilia yake na kumtumia Naira za Nigeria milioni tano (takribani shilingi milioni 16.4 za Tanzania) na kuanzisha mradi wa kumjengea nyumba, na pia ameahidi kumtembelea atakaporudi Nigeria wakati likizo.



# TPLB: Michuano ya Kimataifa imeathiri Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Ligi Kuu, TPLB, imetanabahisha kuwa, michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) imeathiri ratiba ya Ligi Kuu ya NBC.

Hayo yametamkwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo alipoongea jana jijini Dar es Salaam na kuweka wazi kwamba, hakutakuwa na mbinu nyingine zaidi ya kuifanyia mabadiliko ratiba hiyo ya Ligi Kuu.

Kasongo ameyataja mashindano ya CHAN yanayoshirikisha timu za taifa kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani kuwa, ni miongoni yatakayolazimisha mabadiliko ya ligi kuanzia mwezi huu na Januari mwakani.

Mtendaji huyo wa TPLB amesema kuwa, mashindano hayo ya CHAN ambayo Tanzania, Kenya na Uganda zitakuwa nchi mwenyeji, yataanza Januari Mosi mwakani hadi 28, hivyo TPLB italazimika kufanya mabadiliko hayo ya Ligi Kuu ili kuyapisha.

Kabla ya hatua hiyo ya fainali za CHAN, Kasongo amepasha kuwa, kutakwa na mechi za awali kwa timu za mataifa mbalimbali kuwania kufuzu kwa fainali hizo. Michuano hiyo ya awali inaanza mwezi huu wa Oktoba.

Pia Kasongo ameyataja mashindano ya AFCON kama nayo yanawalazimu kufanya mabadiliko ya ratiba ili kutoa nafasi kwa timu yetu ya taifa iliyosheheni wachezaji wengi wanaocheza ligi ya ndani, iendelee kushiriki bila vikwazo.

Ameyataja mashindano mengine yanaweza kuathiriwa na michuano hiyo ya kimataifa ni Kombe la Mapinduzi ambayo hufanyika mwezi Januari kila mwaka.

Kasongo amebainisha kuwa, kipindi hicho cha Januari kinachofanyika Kombe la Mapinduzi, kutakuwa na mechi mfululizo za hatua ya makundi kwa timu za Simba na Yanga zilizotinga hatua hiyo.

"Haya mashindano ya Kombe la Mapinduzi yana wasimamizi na wasemaji wake, naamini watakuja kuliongelea hili, lakini washiriki muhimu Simba na Yanga ndiyo hao kipindi hicho watakuwa kwenye mechi za mfululizo za hatua ya makundi ya mashindano ya klabu barani Afrika," amefafanua Kasongo.

## Rais Brazil ataka wanaocheza nje wasiitwe timu ya taifa

**BLASILIA, Brazil**

RAIS wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva amependekeza kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini hapa kuacha kujumuisha katika kikosi cha timu ya taifa wachezaji wanaocheza soka nje ya Brazil.



Lula da Silva anadai kwamba, wachezaji hao wa sasa hawana ubora kama waliokuwa nao nyota wao wa zamani kama Garrincha na Romario.

Timu ya Taifa ya Brazil kwa sasa iko katika harakati za kufuzu michuano ya Kombe la Dunia 2026 itakayofanyika katika nchi za USA, Mexico na Canada ambapo imekuwa na matokeo ya kusua baada ya kupoteza mchezo wao dhidi ya Paraguay Septemba 11 mwaka huu na Ijumaa iliyopita kupata ushindi wa taabu wa goli 2-1 dhidi ya Chile. Licha ya kikosi hicho kilichopo chini ya kocha Dorival Junior kuwa na mastaa kibao kama Vinicius, Rodrygo, Endrick, Allison, Ederson Moraes, Raphinha na nyota wengine wengi wanaocheza katika vilabu vikubwa barani Ulaya.

"Hao walioko nje sio wazuri kuliko hawa (wanaocheza ndani Brazil), Brazil kuna wachezaji wenye ubora kama wao (wanaocheza nje), hivyo toeni nafasi kwa hawa wanaocheza hapa," alinena Rais Luis.

Rais huyo ambaye anaamini kwa sasa hakuna wachezaji kama Romario au Garrincha waliokuwepo hapo nyuma, anatarajiwa kufanya kikao na rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini hapa CBF, kwa ajili ya mazungumzo zaidi.

# Stars yaendelea kuvurunda nyumbani

## ● Yatafunwa na Chui wa Congo DR mbele ya Majaliwa na Dk. Kikwete

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA ilivyokuwa kwenye mechi dhidi ya Ethiopia iliyolazimisha suluhu na Stars, japo pia Taifa Stars imeshindwa kutumia vema uwanja wa nyumbani kwa kufugwa bao 2-0 na The Leopard ya Congo DR.

Mchezo huo ulianza kipindi cha kwanza kwa Stars kufanya mashambulizi mfululizo kwenye lango la Congo DR 'The Leopard' na kupata kona mbili pacha lakini zote ziliishia kuwa tasa.

Stars iliendelea kuliandama lango la Congo DR na katika dakika ya 6 Clementi Mzize alimtoka beki wao wa kushoto Gedeon Kalulu lakini shuti lake kale lilipanguliwa na kipa wao, Dimitry Bertaud.

Kadiri mpira ulivyoendelea Congo DR walichangamka lakini safu ya ulinzi ya Taifa Stars ikicheza huku jukwaani akiwepo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyekuwa mgeni rasmi wa mechi hiyo, ilikuwa makini na kutibua mipango mingi ya Wacongomani hao.

Dakika ya 11 ya mchezo Congo DR walifanya shambulizi kali lakini kipa Ally Salimu aliokoa mpira huo kwa umaridadi mkubwa.

Stars ilijibu mapigo dakika ya 16 baada ya kiungo Mudathiri Yahya kumpatia pande maridhawa Mbwana Samatta lakini shuti lake likatoka sentimita chache toka lango la Congo DR.

Stars waliendelea kugongeana hapa na pale hususan eneo la katikati ya uwanja lakini walishindwa kumalizia mipango yao vizuri.

Dakika ya 33 ya mchezo The Leopard walifanya shambulizi kali la kushtukiza lakini kwa mara nyingine kipa Salim aliokoa mpira wa tiktaka uliopigwa na mshambuliaji wao, Silas Katompa.

Kibu Denis nusra aipatie Stars bao la kuongoza dakika ya 38 baada ya mpira wake wa kichwa kugonga mwamba na kutoka nje kufuatia krosi safi ya nahodha wa Stars, Samatta.

Kwa mara nyingine Ally Salimu dakika ya 42 alifanya kazi ya ziada kupangua shuti kali la mbali la kiungo wa Leopard, Simon Banza.

Kwa ujumla kipindi hiki Stars ilicheza vema lakini haikuwa na mipango mizuri ya kutengeneza nafasi za kufunga mabao, huku The Leopard wakifanya mashambulizi ya kushtukiza yaliyokuwa hatari sana.

Dakika ya kwanza tu ya mchezo The Leopard walifanya shambulizi kali lakini kwa mara nyingine kipa Salim alidaka kuchwa cha karibu cha Katompa.

Stars ilijibu mapigo dakika ya 3 ya mchezo baada Mudathiri kugongeana vema na Feisal Salumu lakini shuti Feisal anajiandaa kufunga alitokea beki na nahodha wa The Leopard, Chancel Mbemba na kutibua jaribio hilo.

Katika pambano hili la Stars na Leopard, pia alikuwepo uwanjani Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete.

Baada ya kushambuliana kwa zamu, hatimaye dakika ya 87 Tanzania ilipata pigo baada The Leopard kupata bao la kuongoza lililofungwa na Meshack Elia aliyeingia kipindi cha pili.

Katika dakika za majeruhi kiungo mshambuliaji Meshack Elia aliipatia Congo DR bao la pili na kufifisha natumaini ya Watanzania kufuza kwa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON, mwakani kule Morocco.

Hadi dakika tisini zinamalizika Tanzania 0 Congo DR 2.

